ONYO LA MWISHO KWA DUNIA

Mpango wa Ulimwengu Mpya Unakuja!

- Viongozi wa Ulimwengu wanautaka
- Unaungwa mkono na wengi
- Ulitabiriwa miaka 2000 iliyopita
- Umekaribia sana
- Utauteka Ulimwenguwote
- Jinsi ya kuukwepa usiwe mhanga
- Kuanguka kwake ghafula na kwa ukamilifu kulitabiriwa
- Umekuja kwa Wakati wake hasa
- Mpango Mpya wa Kweli

"Tupende au tusipende, tuwe tayari au tusiwe tayari, sisi sote tunaingizwa katika mashindano kamili ya aina tatu ya ulimwengu huu, ambayo hayana kizuizi cho chote kilichowekwa. Hata hivyo, wengi sana miongoni mwetu si washindani. Sisi ni mambo tu zilizopigiliwa njiani. Kwa maana shindano hilo ni juu ya nani atakayeuanzisha mfumo wa kwanza wa serikali ya ulimwengu mzima ambayo haijapata kuwako kamwe katika jamii hii ya mataifa … Shindano hilo ni la kufa na kupona kwa sababu, kwa vile sasa limeanza, basi, hakuna njia yo yote inayoweza kuligeuza au kulisimamisha." Malachi Martin, Mjesuti, azijuaye siri za ndani zaVatikani, *Keys of This Blood*, uk. 15.

Hilo ni wazo kubwa: yaani, huo Mpango wa Ulimwengu mpya, ambao mataifa mbalimbali yanavutwa kuingia pamoja ndani yake kwa kusudi lao moja … ni Marekani peke yake ambayo inayo mambo yote mawili, yaani, msimamo wake kimaadili na uwezo wake wa kuuunga mkono." George Bush, Hotuba yake ya Muungano wa Taifa, *Los Angeles Times*, Feb. 18, 1991.

"Chini ya uongozi shupavu wa Papa Yohane Paulo II, Serikali ya Vatikani imetwaa mahali pake halali katika ulimwengu huu na kuwa sauti ya kimataifa. Ni haki tu kwamba nchi hii ionyeshe heshima yake kwa Vatikani kwa kuitambua kidiplomasia kama Serikali ya Ulimwengu." Dan Quayle, *Appeal to the U.S. Senate*, Sept. 22, 1983.

"(Yohane Paulo II) anasisitiza kwamba wanadamu hawana tumaini lo lote la kutegemewa katika kuunda mfumo wa kisiasa wa ulimwengu mzima ulio na uwezo wa kujitegemea, isipokuwa kama ni kwa kufuata msingi wa Ukristo wa Kikatoliki wa Roma." M. Martin, *Keys of This Blood*, ukurasa 492.

"Umoja wa Mataifa - Viongozi wa mataifa yale yanayounda Baraza la Usalama leo hii walikuwa hapa New York kwa mkutano wao wa kwanza wa wakuu wa nchi, wakiwa tayari kuuweka Umoja wa Mataifa kuwa sehemu muhimu sana ya mpango huu wa ulimwengu mpya na kuunda sera ya pamoja juu ya kuleta amani na kudhibiti silaha…. "Mkutano huo wa viongozi wa mataifa hayo 15 yaliyomo katika Baraza la Usalama unaweka kumbukumbu kwa mara yake ya kwanza tangu kuundwa kwa shirika hilo la ulimwengu mwaka 1945,

Baraza hilo, likiwa ni kiungo chenye nguvu kuliko vyote cha Umoja wa Mataifa, limefanya mkutano wake katika ngazi yake ya juu kabisa." *Birmingham News*, Jan. 31, 1992.

"Wale miongoni mwetu walio chini ya miaka sabini angalau wataona ukiwekwa msingi wa mfumo huo wa serikali ya ulimwengu mpya. Wale miongoni mwetu walio chini ya miaka arobaini kwa hakika wataishi chini ya mamlaka ya bunge, serikali, na sheria yake, pamoja na utawala wake. Naam, washindani hao watatu [George Bush, Papa Yohane Paulo II, na Mikhail Gorbachev] - pamoja na wengine wengi zaidi kando ya hao, kwa kadiri wakati unavyosonga mbele - wanaongea juu ya huo Mpango wa Ulimwengu Mpya si kama kitu kinachokuja kwenye kona iliyo mbali sana ya wakati, bali kama kitu kilicho karibu sana kutokea." M. Martin, *Keys of This Blood*, uk. 15-16.

"Hiyo ndiyo ndoto juu ya Mpango huo. Kama yalivyo mawazo mengi ya kimapinduzi, Ulaya Iliyoungana Pamoja si wazo jipya, bali ni la zamani ambalo limefufuliwa tena. Ndoto hiyo ya kuwapo kwa mpango huo na umoja ambayo zamani ilikuwamo katika Roma ile ya Makaisari, iliendelea kuwako kupitia katika kipindi kile cha Zama za Kati (kipindi kiitwacho Zama za Giza kwa usahihi) sio tu katika Kanisa la Katoliki la Roma, bali katika ile Dola Takatifu ya Roma." *Time*, Okt. 6, 1961.

"Kile kilichoundwa chini ya Mkataba wa Roma katika Soko lao la Pamoja ni urasimu mpya uliounganishwa kikiki, uliowekwa kikiki chini ya makao makuu, unaoongozwa kikiki, unaotawaliwa kikiki, ambao kwa dhahiri unajaribu kuurejesha tena kule Ulaya ule mfumo wa uchumi uliokuwako katika ile Dola Takatifu ya Roma." *Christian Science Monitor*, 1962.

Marekani – Upapa – Umoja wa Mataifa

Si kusudi la makala hii kuwashambulia watu binafsi, bali kusimulia kidogo historia ya mambo ya mbele ambayo yalitabiriwa katika Biblia kuhusu Mfumo huo au Dini hiyo ya Kikatoliki.

Je, Roma
Itatawala Ulimwengu Tena?

KANISA LA MTAKATIFU PETRO, ROMA

Maridhiano ya Kufisha

Mtume Paulo, katika Waraka wake wa Pili kwa Wathesalonike, alitabiri juu ya uasi mkuu ambao ungeleta matokeo ya kuianzisha mamlaka ile ya upapa. Alitangaza kwamba siku ile ya kuja Kristo isingeweza kuja, "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa mtu yule wa dhambi (kuasi), mwana wa uharibifu; yule Mpingamizi [Mpinga Kristo], ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu [kanisa] la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Tena, zaidi ya hayo, Mtume huyo anawaonya ndugu zake kwamba "ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi." 2 Wakorintho 2:3,4,7. Hata katika kipindi kile cha mwanzo kabisa aliona yakiingia ndani ya kanisa mafundisho potofu ambayo yangetayarisha njia ya kujitokeza kwa upapa.

Kidogo kidogo, mwanzoni kwa siri na kimya kimya, na baadaye kwa wazi zaidi, ikaongezeka nguvu yake na kuitawala mioyo ya wanadamu, ile "siri ya kuasi" ikaiendeleza mbele kazi yake kwa kutumia madanganyo na makufuru. Karibu bila kutambulikana kabisa desturi zile za kikafiri zikaingia ndani ya kanisa la Kikristo. Roho ile ya maridhiano na kufanana-fanana [na dunia] ilizuiwa kwa wakati fulani kutokana na mateso makali ambayo kanisa lilistahimili chini ya wapagani. Lakini mateso yale yalipokoma, na Ukristo ulipoingia katika mabaraza na majumba ya kifalme, ndipo kanisa lile lilipouweka kando unyenyekevu ule wa Kristo na Mitume wake na kujitwalia ufahari na kiburi cha makuhani na watawala wale wa kipagani; na mahali pa matakwa ya Mungu likaweka nadharia za

wanadamu pamoja na desturi zao. Kuongoka kwa jina tu kwa Konstantino, mapema katika karne ile ya nne, kulileta shangwe kubwa; na ulimwengu [upagani], ukiwa umevikwa joho la mfano wa haki, ukatembea na kuingia ndani ya kanisa. Basi, kazi ile ya uharibifu ikasonga mbele kwa haraka sana. Upagani, wakati ukionekana kana kwamba umeshindwa kabisa, ukawa ndio mshindi. Roho yake ikalitawala kanisa lile. Mafundisho yake ya dini, sherehe zake, na ushirikina wake vikaingizwa katika imani na ibada ya wale waliojidai kuwa ni wafuasi wake Kristo.

Mtu wa Dhambi

Maridhiano hayo kati ya Upagani na Ukristo yalikuwa na matokeo ya kujitokeza kwa “mtu yule wa dhambi” (man of sin) ambaye alitabiriwa katika unabii huo kuwa atakuwa Mpingamizi [Mpinga Kristo], na ya kwamba atajiinua mwenyewe juu ya Mungu. Mfumo huo mkubwa kabisa wa dini ya uongo ni kazi kuu ya kilele ya uwezo wake Shetani - yaani, ni kielelezo bora kabisa cha kazi ile inayostahili kukumbukwa ambayo inatokana na juhudi zake [Shetani] za kujiketisha yeye mwenyewe juu ya kiti cha enzi ili kuitawala dunia hii kama apendavyo yeye.

Siku moja Shetani alijitahidi sana kufanya maridhiano na Kristo. Akaja kwa Mwana wa Mungu katika nyika ile ya majaribu, na kumwonyesha falme zote za dunia hii pamoja na utukufu wake, na kujitolea kumpa vyote mikononi mwake mradi tu akubali kwamba mkuu yule wa giza [Shetani] ndiye mwenye mamlaka yote. Kristo alimkemea mjaribu yule mwenye kiburi na kumlazimisha kuondoka pale. Lakini Shetani anapata mafanikio makubwa sana anapoyaleta majaribu yale yale kwa mwanadamu. Ili kujipatia manufaa na heshima za ulimwengu huu, kanisa lile likatafuta upendeleo na kuungwa mkono na wakuu wa dunia hii; na kwa njia hiyo, likiwa limemkana Kristo, likashawishiwa kutoa utii wake kwa mwakilishi yule wa Shetani - yaani, kwa Askofu [Papa] yule wa Roma.

Msingi wa Fundisho Hilo la Uongo

Ni mojawapo la mafundisho makuu ya dini ile ya Kiroma kwamba papa ni kichwa kinachoonekana kwa macho cha kanisa la ulimwengu mzima la Kristo, kwamba amepewa mamlaka ya juu kabisa juu ya maaskofu na wachungaji wote katika sehemu zote za dunia hii. Zaidi ya hayo, papa amepewa vyeo vya Mungu. Amepewa cheo cha "Bwana Mungu Papa," tena ametangazwa kuwa hawezi kukosea kamwe. Anadai kwamba wanadamu wote wanapaswa kumsujudu yeye. Dai lile lile alilolisisitiza Shetani katika nyika ile ya majaribu bado linasisitizwa naye [papa] kupitia katika Kanisa la Roma, na idadi kubwa sana ya watu wako tayari kumsujudu yeye.

"Tunashikilia hapa duniani
mahali pa
Mungu Mwenyezi."
Papa Leo wa 13,
Katika Barua yake ya Utume,
Juni 20, 1894.

Lakini wale wanaomcha na kumheshimu Mungu, kama vile Kristo alivyopambana na ubembelezi wa yule adui mwerevu, wanapambana na madai hayo yatokanayo na ushupavu wake wa kujinyakulia vyeo vya Mungu, wakisema: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Luka 4:8. Mungu hajatoa dokezo lo lote katika Neno lake

lisemalo kwamba amemchagua mwanadamu fulani kuwa kichwa cha kanisa lake. Fundisho la dini la ukuu wa papa usio na kifani hupingana moja kwa moja na mafundisho ya Maandiko. Papa hawezi kuwa na mamlaka yo yote juu ya Kanisa la Kristo isipokuwa kwa utapeli.

Wafuasi wa papa wamekazana sana kuleta mashtaka ya uzushi dhidi ya Waprotestanti na dhidi ya kujitenga kwao kwa makusudi toka katika kanisa lao la kweli. Lakini mashtaka hayo ndiyo hasa yanayowahusu wao wenyewe. Wao ndio walioitupa chini bendera ya Kristo na kujitenga mbali na ile "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Yuda 3.

Mgunduzi wa Mafundisho ya Uongo

Shetani alijua fika ya kwamba Maandiko yale Matakatifu yangewawezesha wanadamu kuyang'amua madanganyo yake na kuupinga uwezo wake. Ilikuwa ni kwa njia ya Neno hilo hata yule Mwokozi wa ulimwengu aliweza kuyapinga mashambulio yake. Kwa kila shambulio lake [Shetani], Kristo alionyesha ngao ya ile kweli ya milele, akisema, "Imeandikwa." Kwa kila shauri alilotoa yule adui, alikataa kwa kutegemea hekima na uwezo wa lile neno. Ili huyo Shetani apate kudumisha utawala wake juu ya wanadamu, na kuimarisha mamlaka ya tapeli yule wa kipapa, ilikuwa ni lazima kwake kuwaweka watu katika hali ya ujinga wa kutoyajua Maandiko. Biblia ingemtukuza Mungu na kuwaweka wanadamu mahali pao panapowastahili hasa; kwa hiyo ilikuwa ni lazima kwamba zile kweli zake takatifu zifichwe kwa watu na kupigwa marufuku. Mantiki hiyo ikatumiwa na Kanisa la Roma. Kwa mamia ya miaka uenezaji wa Biblia ulipigwa marufuku. Watu walikatazwa kuisoma au kuwa nayo katika nyumba zao, na makasisi (mapadre) pamoja na maaskofu wapotovu wakayafafanua mafundisho yake ili yapate kuunga mkono unafiki wao. Hivyo ndivyo papa alivyokuja kutambulikana karibu ulimwenguni kote kama Kaimu wa [Aliye Badala ya] Mungu hapa duniani, ambaye alipewa mamlaka juu ya kanisa na serikali.

Kuelewa Unakokwenda Upapa, Angalia Historia

Yake Iliyopita

Kuupigia Magoti Upagani

Baada ya kuondolewa yule anayegundua mafundisho potofu [yaani, Biblia], Shetani akafanya kama apendavyo. Unabii ulikuwa umetangaza kwamba upapa unge“azimu kubadili majira na Sheria [Amri Kumi].” Danieli 7:25. Kazi hiyo [upapa] haukuchelewa kuanza kuifanya. Ili kuwapa waongofu waliotoka kwenye upagani kitu fulani badala ya ibada yao ya sanamu, na kukuzia upokeaji wao wa Ukristo kwa jina tu, kuabudu sanamu na mabaki ya mifupa ya watakatifu waliokufa zamani vikaingizwa taratibu katika ibada ya Kikristo. Amri iliyotolewa na baraza kuu hatimaye ikauimarisha mfumo huo wa ibada ya sanamu. Kuikamilisha kazi hiyo ya kukufuru, Roma ikadhamiria kuifutilia mbali kutoka katika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] amri ile ya pili inayokataza ibada ya sanamu, na kuigawa amri ile ya kumi ili kuhifadhi idadi ile ile [ya Amri Kumi].

SHERIA YA MUNGU

I

Usiwe na miungu mingine ila mimi.

II

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu Mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudu wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu Wanipendao, na kuzishika amri zangu.

III

Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

IV

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; Lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya Mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; Kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

V

Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.

VI

Usiue.

VII

Usizini.

VIII

Usiibe.

IX

Usimshuhudie jirani yako uongo.

X

Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako, mtumwa wake, wala mjakazi , wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.

Kutoka 20:3-17.

SHERIA YA MUNGU

KAMA ILIVYOBADILISHWA NA MWANADAMU

I
Mimi ni Bwana Mungu wako,
Usiwe na miungu migeni ila mimi.
(Amri ya Pili Imeachwa.)

II
(Hii hasa ni ya III)
Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako.

III
(Hii hasa ni ya IV)
Kumbuka kwamba unaitakasa siku ya Sabato.
(Amri ya Sabato imebadilishwa vibaya sana!)

IV
(Hii hasa ni ya V)
Waheshimu baba na mama yako.

V
(Hii hasa ni ya VI)
Usiue.

VI
(Hii hasa ni ya VII)

Usizini.

VII
(Hii hasa ni ya VIII)
Usiibe.

VIII
(Hii hasa ni ya IX)
Usimshuhudie jirani yako uongo.

IX
(Hii hasa ni ya X, Sehemu ya Kwanza)
Usimtamani mke wa jirani yako.

X
(Hii hasa ni ya X, Sehemu ya Pili)
Usitamani mali ya jirani yako.

Katekisimu ya Wote ya Kikatoliki.

Maridhiano Yaendelea

Roho ile ya maridhiano na upagani ikafungua njia ya kutoijali sana Mamlaka ile ya Mbinguni. Shetani, akifanya kazi yake kwa kuwatumia viongozi wa kanisa wasiojitoa wakf kwa Mungu, akaigeuza amri ile ya nne pia, na kujaribu kuiweka kando Sabato ile ya kale [Jumamosi], siku ambayo Mungu alikuwa ameibarikia na kuitakasa, na mahali pake kuitukuza sikukuu iliyoadhimishwa na makafiri kama "siku tukufu ya jua" [Jumapili]. Badiliko hilo mwanzoni halikufanywa waziwazi. Katika karne zile za mwanzo Sabato ya kweli [Jumamosi] ilikuwa imetunzwa na Wakristo wote. Walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima ya Mungu, na, wao wakiwa wanaamini kwamba Sheria ya Mungu [Amri Kumi] haibadiliki kamwe, basi, kwa bidii nyingi walitunza utakatifu wa amri zake [kumi]. Lakini kwa ussiri mkubwa Shetani alifanya kazi yake kupitia kwa vibaraka wake ili kutekeleza lengo lake. Ili mawazo ya watu yapate kugeuzwa kuelekea kwenye ile Jumapili, ikafanywa kuwa sikukuu ya kuheshimu ufufuo wa Kristo. Ibada za dini zikaendeshwa kataika siku hiyo; lakini bado ilifikiriwa kama siku ya mapumziko tu, Sabato [Jumamosi] ikiwa inaendelea kutakaswa.

Kutayarisha njia kwa ajili ya kazi ile aliyokusudia kuifanya, Shetani akawaongoza Wayahudi, kabla ya kuja kwa Kristo, kuiwekea Sabato mizigo mizito na masharti makali, wakifanya utunzaji wake kuwa mzigo mzito ulemeao. Basi, [Shetani] akiitumia nafasi hiyo ya kuwapo kwa nuru ile ya uongo ambayo kwayo aliifanya [Sabato] ifikiriwe vibaya, akaifanya ipate kudharauliwa na watu kama siku ya Wayahudi.

Wakati Wakristo wakiendelea kwa kawaida kuiadhimisha Jumapili kama sikukuu ya furaha, akawaongoza kuifanya siku ya Sabato [Jumamosi] kuwa siku ya kufunga [saumu], yaani, siku ya huzuni na majonzi, ili kuonyesha chuki yao dhidi ya dini ile ya Kiyahudi.

Badiliko la Kijasiri

Katika sehemu ile ya kwanza ya karne ya nne mfalme Konstantino alitoa amri na kuifanya Jumapili kuwa sikukuu ya serikali katika dola yote ya Waroma. Siku hiyo ya jua [Jumapili] iliheshimiwa na raia zake wapagani, tena iliheshimiwa na Wakristo; ilikuwa ni sera ya mfalme yule kuunganisha mambo yale waliyoyapenda makafiri na Wakristo ambayo yalikuwa yanaleta mgongano. Alishurutishwa kufanya hivyo na maaskofu wa kanisa, wakiwa wamechochewa na tamaa ya ukuu na kiu ya mamlaka walitambua kwamba kama siku ile ile moja ingeadhimishwa na Wakristo na makafiri, basi, ingeweza kusaidia kupokelewa kwa Ukristo na wapagani wale na kwa njia hiyo kuendeleza mbele mamlaka na utukufu wa kanisa. Lakini Wakristo wengi wacha Mungu waliposhawishiwa polepole kuifikiria Jumapili kama ina kiwango fulani cha utakatifu, bado waliendelea kuitunza Sabato ya kweli [Jumamosi] kama takatifu kwa Bwana, tena waliitunza kwa kutii amri ile ya nne [Kut. 20:8-11].

Laghai yule mkuu [Shetani] alikuwa bado hajaikamilisha kazi yake. Akaazimu kuukusanya pamoja Ulimwengu wote wa Kikristo chini ya bendera yake na kutumia uwezo wake kupitia kwa kaimu wake, yaani, yule papa, mwenye majivuno mengi, aliyejidai kwamba alikuwa ndiye mwakilishi wake Kristo. Kupitia kwa wapagani wale walioongoka nusu-nusu, na kwa maaskofu wale wenye kutaka makuu, na kwa watu wa kanisa walioipenda dunia akalitimiza kusudi lake. Mabaraza makubwa sana yakafanywa toka wakati hata wakati, na katika hayo viongozi wakuu wa kanisa walikutana kutoka pande zote za

ulimwengu. Karibu katika kila baraza lililokaa, Sabato [Jumamosi] ambayo Mungu alikuwa ameianzisha ikasukumiwa chini kidogo zaidi, wakati ule ule Jumapili ikawa inainuliwa juu. Hivyo ndivyo sikukuu ile ya kipagani [Jumapili] ilivyokuja kuheshimiwa hatimaye kama siku iliyowekwa na Mungu, na wakati ule ule Sabato ile ya Biblia [Jumamosi] ikatangazwa kuwa ilikuwa ni mabaki ya dini ile ya Kiyahudi, na watunzaji wake wakatangazwa kuwa wamelaaniwa.

"Jumapili imewekwa na Wakatoliki, na madai ya kutaka itunzwe yanaweza tu kutetewa kwa kufuata kanuni za Kikatoliki….Toka mwanzo hadi mwisho wa Maandiko Matakatifu hakuna kifungu hata kimoja kinachotoa kibali cha kuhamisha ibada ya kila juma kutoka katika siku ile ya mwisho wa juma kwenda ile ya kwanza." *Catholic Press*, **Sydney, Australia, Agosti, 1900.**

Muhuri wa Muumbaji Waondolewa

Mwasi huyo mkuu alikuwa amefanikiwa kujiinua mwenyewe “juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa.” 2 Wathesalonike 2:4. Akadiriki kuibadili amri ile ya pekee katika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ambayo bila kukosea hata kidogo inawaelekeza wanadamu wote kwa Mungu wa kweli, aliye hai. Katika amri ile ya nne [Kut. 20:8-11] Mungu anadhihirishwa kama ndiye Muumbaji wa mbingu na nchi, na kwa sababu hiyo yeye anatofautishwa na miungu yote ya uongo. Ilikuwa ni kwa ajili ya kumbukumbu ya kazi ile ya uumbaji, ndiyo maana siku ile ya saba [Jumamosi] ilitakaswa [ilitengwa kwa matumizi matakatifu] kama siku ya mapumziko kwa kila mwanadamu. Ilikusudiwa kumweka Mungu aliye hai daima kataika mawazo ya wanadamu kama chimbuko la uhai wao na lengo la kicho chao na ibada yao. Shetani anajitahidi sana iuwageuza watu waache kumtii Mungu, na kuacha kutoa utii wao kwa Sheria yake [Amri Kumi]; kwa hiyo, juhudi zake anazielekeza hasa dhidi ya amri ile [ya Sabato] inayomwonyesha Mungu kuwa ni Muumbaji.

Waprotestanti siku hizi wanasisitiza kwamba ufufuo wake Kristo katika siku ile ya Jumapili ndio ulioifanya siku hiyo kuwa Sabato ya Kikristo. Lakini ushahidi wa Maandiko unakosekana. Hakuna heshima kama hiyo iliyotolewa kwa siku hiyo [ya Jumapili] na Kristo au na Mitume wake.

Toka Roma ya Kipagani Kwenda Roma ya Kipapa

Katika karne ile ya sita upapa ulikuwa umejiimarisha sana. Kiti chake cha enzi kilikuwa katika mji ule wa dola [Roma], na Askofu wa Roma [Papa] akatangazwa kuwa ndiye kichwa cha kanisa lote. Upagani ukaupa upapa nafasi yake [Dan. 8:12; 12:11]. Yule Joka [Ibilisi na Roma ya Kipagani – Ufu. 12:9,3] alikuwa amempa mnyama [mfalme – Dan. 7:17] "nguvu zake na kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi." Ufunuo 13:2. Na sasa ikaanza ile miaka 1260 ya mateso [mauaji] ya papa yaliyokuwa yametabiriwa katika unabii wa Danieli na Ufunuo. Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7. Wakristo wakalazimishwa ama kuuacha msimamo wao mnyofu na kuzikubali sherehe za kipapa pamoja na ibada yake, ama kuchomwa moto juu ya kitita cha kuni, ama kukabiliwa na mtu yule akataye vichwa kwa shoka. Basi, maneno ya Yesu yakawa yametimizwa, aliyosema: "Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha [watawaua] baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu." Luka 21:16,17. Mateso yakaanzishwa rasmi dhidi ya wale waliokuwa waaminifu kwa ukali sana kuliko wakati wo wote uliopita, na dunia hii ikawa ni uwanja mkubwa wa vita. Kwa mamia ya miaka Kanisa la Kristo likapata kimbilio lake katika maeneo ya upweke na ya siri. Nabii yule asema hivi: "Yule mwanamke [Kanisa la Kristo la Kweli] akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko kwa muda wa siku [miaka – Eze. 4:6] elfu na mia mbili na sitini." Ufunuo 12:6.

Katika Karne Zile za Mwanzo Sabato ya Kweli

Ilitunzwa na Wakristo Wote.

ZAMA ZA GIZA ZAANZA

Kule kujipatia mamlaka yake lile Kanisa la Roma ndio mwanzo wa Zama za Giza. Kadiri uwezo wake ulivyozidi kuongezeka, ndivyo giza [yaani, ujinga wa kutoijua Biblia, Sayansi na Teknolojia] lilivyozidi kuwa nene. Imani ikahamishwa kutoka kwa Kristo, aliye msingi wa kweli, kwenda kwa papa wa Roma. Badala ya kumtegemea Mwana wa Mungu kwa msamaha wa dhambi na wokovu ule wa milele, watu wakamtazama papa, na makasisi (mapadre) na maaskofu ambao alikuwa amewakabidhi mamlaka. Wakafundishwa ya kwamba papa alikuwa ndiye mpatanishi wao wa kibinadamu na ya kwamba hakuna hata mmoja ambaye angeweza kumwendea Mungu isipokuwa kwa kupitia kwake, na kwa ajili hiyo yeye alipaswa kupewa utii bila swali lo lote. Kwenda kinyume na matakwa yake ilikuwa ni sababu ya kutosha ya kutolewa adhabu kali sana juu ya miili na roho za wale wahalifu. Kwa njia hiyo, mawazo ya watu yakageuziwa mbali na Mungu na kuelekezwa kwa wanadamu wawezao kukosa, kupotoka, na wakatili, naam, zaidi sana, kwa yule mkuu wa giza mwenyewe [Shetani], ambaye alitumia uwezo wake kupitia kwa watu wale. Dhambi ikafichwa katika vazi la utakatifu. Maandiko yanapozuiwa kusomwa na watu, na mwanadamu anapokuja kujiona mwenyewe kuwa ni mkubwa kuliko wote, hapo ndipo tunapohitaji tu kutazamia kuona hila, udanganyifu, na uovu unaoishusha hadhi ya mwanadamu. Katika kuzitukuza sheria za wanadamu na mapokeo ukaonekana ufisadi ambao hutokea daima wakati Sheria ya Mungu [Amri Kumi] inapowekwa kando.

Siku za Hatari Kubwa

Zile zilikuwa ni siku za hatari kubwa kwa Kanisa lake Kristo. Waaminifu walioibeba bendera yake walikuwa ni wachache kweli kweli. Ingawa ile kweli haikuachwa bila kuwapo mashahidi, hata hivyo, wakati fulani ilionekana kana kwamba mafundisho yale ya uongo na ushirikina yalikuwa yameenea kote, na dini ile ya kweli ilionekana kana kwamba ingeweza kufutiliwa mbali duniani kote. Injili ikawa imesahauliwa, lakini mitindo ya dini ikaongezeka, na watu wakawa wamelemewa na mizigo mizito waliyotwishwa yenye masharti makali.

Wakafundishwa sio tu kumtazama papa kama ndiye mpatanishi wao, bali kutegemea matendo yao wenyewe ili kuweza kulipa fidia ya dhambi zao. Safari ndefu za taabu kwenda kuzuru patakatifu, kutenda matendo ya kitubio, kuabudu mifupa ya watakatifu waliokufa zamani, kujenga makanisa, kujenga makaburi ya watakatifu, na altare [madhabahu], kulipa fedha nyingi kwa kanisa - mambo hayo pamoja na matendo mengine yanayofanana na hayo yaliamriwa ili kuituliza ghadhabu ya Mungu au kupata upendeleo wake, kana kwamba Mungu alikuwa kama wanadamu, kuweza kukasirishwa kwa mambo madogo sana yasiyo na maana, au kutulizwa kwa kupewa zawadi au kwa maungamo (kitubio)!

Giza lile likaonekana kana kwamba lilikuwa likiongezeka kuwa nene zaidi. Ibada ya sanamu ikawa ni jambo

la kawaida kwa watu wengi. Mishumaa ikawashwa mbele ya sanamu zile na sala zikatolewa kwa sanamu zile. Desturi zile za kipuuzi kabisa na za kishirikina, hata akili zao zenyewe zikaonekana kana kwamba zimepoteza uwezo wake wa kujitawala. Wakati wale makasisi (mapadre) na maaskofu wenyewe walikuwa wanapenda anasa, uasherati, na ufisadi, iliweza kutazamiwa tu kwamba, watu wale waliowategemea kwa uongozi wao, nao wangeweza kuzama katika ujinga na uovu wao.

Papa yule Mwenye Majivuno

Hatua nyingine katika dhana za kipapa ilichukuliwa katika karne ile ya kumi na moja wakati Papa Gregori wa Saba alipotangaza ukamilifu wa Kanisa la Roma. Miongoni mwa mawazo yake aliyotoa lilikuwapo wazo moja lililosema kwamba kanisa lile [la Roma] lilikuwa halijapata kukosea kamwe kulingana na Maandiko. Lakini ushuhuda wa Maandiko hayo haukuambaatana na lile dai lake. Papa yule mwenye majivuno mengi alidai pia kwamba anao uwezo wa kuwaondoa wafalme katika kiti chao cha enzi, kisha akatangaza kwamba hakuna hukumu yo yote aliyoitoa yeye ambayo ingeweza kubatilishwa [kugeuzwa] na mtu ye yote, ila kwamba yeye ndiye alikuwa na haki ya kuyabatilisha [kuyageuza] maamuzi ya wengine wote.

Ni tofauti kubwa ya kushangaza mno jinsi gani kati ya kiburi kile kilichojaa uonevu cha papa yule mwenye majivuno mengi ukilinganisha na upole na unyenyekevu wa moyo aliokuwa nao Kristo, ambaye anajiwakilisha mwenyewe kama mmoja anayebisha katika mlango wa moyo akiomba kuingia ndani, ili apate kuingia humo na kuleta msamaha na amani, na ambaye aliwafundisha wanafunzi wake, akasema: “Na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu.” Mathayo 20:27.

Giza Lazidi Kuwa Nene

Karne zile zilipozidi kusonga mbele zilishuhudia ongezeko la daima la uongo katika mafundisho ya dini yaliyotolewa kutoka Roma. Hata kabla ya kuanzishwa kwa upapa mafundisho ya wanafalsafa wale makafiri yalikuwa yamezingatiwa, nayo yalitoa mvuto wake ndani ya kanisa. Wengi waliodai kwamba wameongoka walikuwa bado wanazing'ang'ania itikadi za falsafa yao ya kipagani, na si kwamba tu waliendelea kujifunza falsafa hiyo wao wenyewe, bali waliwashurutisha wengine kuipokea kama njia ya kueneza mvuto wao miongoni mwa makafiri wale. Makosa mazito yakaingizwa kwa njia hiyo katika imani ya Kikristo. Lililojitokeza sana katika hayo ni ile imani kwamba mwanadamu ana roho isiyokufa, na ya kwamba, akifa bado anaendelea kuwa na fahamu zake. Fundisho hilo la dini likaweka msingi ambao juu yake Roma ilianzisha sala kwa ajili ya watakatifu waliokufa na ibada ya Bikira Maria. Kutokana na fundisho hilo pia ukazuka uzushi uliosema kwamba wale ambao hatimaye hawataweza kutubu wataendelea kuteswa motoni milele hata milele, fundisho ambalo liliingizwa katika imani ya kipapa.

Ndipo njia ikawa imetayarishwa ya kuingizwa [kanisani] mavumbuzi mengine ya kipagani ambayo Roma iliyaita kwa jina la 'Toharani' (purgatory), nao wakalitumia fundisho hilo kuwatisha makundi ya watu wale waliokuwa wajinga na washirikina. Kwa uzushi wao huo, wanathibitisha kwamba pako mahali pa mateso, ambapo roho za wale wasiostahili adhabu ya milele zinapaswa kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, na ya kwamba, kutoka hapo, zinapowekwa huru mbali na uchafu wake, roho hizo huingizwa mbinguni.

Mtazamo wa Kifedha

Bado ikawapo haja ya kubuni uongo mwingine ili kuiwezesha Roma kunufaika kutokana na hofu hiyo na maovu ya wafuasi wake. Uongo huo uliwezekana kwa fundisho lao la indulgensia [ondoleo la dhambi]. Ondoleo kamili la dhambi, zilizopita, za sasa, na za baadaye, na kuachiliwa ili mtu asiweze kupatikana na maumivu yote pamoja na adhabu anazostahili [toharani], wakawa wameahidiwa kupewa wale wote ambao wangejiandikisha katika vita vya papa ili kupanua mipaka ya utawala wake wa kidunia, ili kuwaadhibu maadui zake, au kuwaangamiza kabisa wale ambao wangethubutu kuupinga ukuu wake usio na kifani. Watu walifundishwa pia kwamba kwa kulipa fedha kwa kanisa wangeweza kujiweka huru mbali na dhambi, na pia kuzifungua roho za marafiki zao waliokufa zilizokuwa zimefungiwa katika moto ule wa mateso. Kwa njia kama hizo Roma ilijaza makasha yake kwa fedha na kuendeleza ufahari, anasa, na uovu wa wale wawakilishi wanafiki wa yeye [Kristo], ambaye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake.

"Papa si mwakilishi tu wa Yesu Kristo, bali yeye ndiye Yesu Kristo, aliyejificha katika vazi la mwili."
The Catholic National, Julai 1895.

Muumbaji Aumbwa

Agizo la Maandiko kuhusu Meza ya Bwana lilikuwa limeondolewa na mahali pake ikawekwa ibada ya sanamu ya Misa. Makasisi (mapadre) wa kikatoliki, kwaa kutamka maneno fulani ya kidini yasiyo na maana, wakajifanya kuwa wanaweza kuugeuza mkate wa kawaida na divai kuwa "mwili na damu [halisi] ya Kristo." - Kadinali Wiseman, *The Real Presence of the Body and Blood of Our Lord Jesus Christ in the Blessed Eucharist, Provede From Scripture*, hotuba ya 8, Sehemu ya 3, aya ya 26. Kwa kiburi chao cha makusudi kabisa kilichojaa makufuru, walidai waziwazi kwamba wanao uwezo wa kumwumba Mungu, Muumbaji wa vitu vyote. Wakristo walitakiwa, kwa tishio la kifo, kukiri imani yao katika uzushi huo wa kutisha unaoitukanisha Mbingu. Watu wengi waliokataa walitupwa motoni.

Mamilioni ya Wafiadini

Katika karne ile ya kumi na tatu kilianzishwa chombo cha papa cha kutisha mno, - yaani, ile Inkwizisheni [Mahakama ya Kanisa Katoliki ya kukomesha uasi]. Mkuu yule wa giza alifanya kazi yake pamoja na viongozi wa utawala huo msonge wa kipapa. Katika mabaraza yao ya siri Shetani na malaika zake waliyatawala mawazo ya watu wale waovu, ijapokuwa alikuwa haonekani kwa macho, malaika wa Mungu alikuwa amesimama katikati yao, akichukua kumbukumbu ya kutisha ya amri zao zilizojaa uovu na kuandika historia ya matendo yao ya kutisha mno kuweza kuonwa kwa macho ya kibinadamu. "Babeli Mkuu" [Roma] alikuwa "amelewa na damu ya watakatifu." Miili ya mamilioni ya wafiadini iliyokuwa imeharibiwa vibaya ikamlilia Mungu ili apate kulipiza kisasi kwa mamlaka hiyo asi.

"Papa Yohane Paulo II aliomba msamaha kwa ajili ya vita iliyopiganwa kule Ulaya kati ya Wakatoliki na Waprotestanti katika kipindi kile cha Upingaji wa Matengenezo ya Kanisa Counter-Reformation)."
U. S. News and World Report, **Julai 3, 1995.**

Taarifa za habari hii pamoja na habari nyingine zinazofanana na hii n i kukiri uwajibikaji kwa mauaji ya mamilioni ya wafiadini katika kipindi kile cha za Giza kwa kutumia njia ya mzunguko. Biblia inatabiri kwamba chini ya hali zile za dhiki zilizo mbele yetu hivi sasa, Upapa na wale wanaouunga mkono watatumia tena nguvu za dola (serikali) kuwadhibiti wale wasiokubaliana na mafundisho yao ya dini.

****

"Kwa kukiri imani iliyo kinyume na Kanisa la Roma, historia inaweka kumbukumbu ya wafiadini zaidi ya watu milioni mia moja." *Brief Bible Readings*, **ukurasa 16.**

"Tarehe 24 Agosti, 1527, Wakatoliki wa Roma kule Ufaransa, kwa mpango uliokuwa umepangwa mapema chini ya uongozi wa Majesuti, waliwaua Waprotestanti 70,000 Katika kipindi cha miezi miwili. Papa alishangilia sana kusikia matokeo hayo yaliyofaulu." *Western Watchman*, **Novemba, 21, 1912, (La Kikatoliki).**

"Kwamba hilo Kanisa la Roma limemwaga damu nyingi sana isiyo na hatia kuliko taasisi nyingine yo yote iliyopata kuwako miongoni mwa binadamu, jambo hilo halitaweza kutiliwa mashaka yo yote na Mprotestanti ye yote aliye na ujuzi wa kutosha wa Historia…. Haiwezekani kabisa kuwa na dhana kamili ya idadi kubwa ya wahanga wake waliouawa ." W. E. H. Lecky, *History of the Rise and Influence of the Spirit of Rationalism in Europe*, gombo la 2, ukurasa 32, toleo la 1910.

"Inakadiriwa … wastani wa mauaji ya kidini ya watu 40,000 kwa kila mwaka wa kuwako kwa Upapa." John Dowling, *The History of Romanism*, ukurasa 541-542. [Upapa ulitawala miaka 1260 kuanzia 538 B.K. hadi 1798 B.K. Kwa hiyo makadirio ya chini kabisa ya wafiadini waliouawa na Kanisa la Roma ni 1260 x 40,000 = 50,400,000.]

Giza Totoro

Upapa ukawa dikteta dhalimu wa ulimwengu mzima. Wafalme na Wafalme Wakuu wa Dola wakazipigia magoti amri za papa wa Roma. Hatima ya maisha ya watu, kwa wakati huu wa sasa na kwa milele zote, ikaonekana kana kwamba ilikuwa chini ya udhibiti wake. Kwa mamia ya miaka mafundisho ya dini kutoka Roma yalikuwa yameenezwa katika mapana yote na kupokewa na watu bila maswali, taratibu zake za ibada zikaendeshwa kwa kicho, sikukuu zake zikatunzwa na watu wote. Makasisi wake wakapewa heshima na kupewa mahitaji yao ya kimwili kwa wingi. Kanisa la Roma halijapata kamwe kufikia heshima kuu, ufahari, au mamlaka kuu kama ile.

Maovu Yaliyoachiliwa Bila Kuzuiwa

Lakini ile "adhuhuri ya upapa ikawa ni usiku wa manane kwa ulimwengu mzima." - J. A. Wylie, *The History of Protestantism*, kitabu cha 1, sura ya 4. Maandiko Matakatifu yalikuwa karibu hayajulikani kabisa, si kwa watu wa kawaida tu, bali kwa makasisi pia. Kama Mafarisayo wale wa zamani, viongozi wale wa kipapa waliichukia nuru ambayo ingeweza kuzifichua dhambi zao. Sheria ya Mungu [Amri Kumi], yaani, ile kanuni ya haki, baada ya kuondolewa, wakatumia mamlaka yao bila kikomo, na kutenda maovu bila kujizuia. Hila, uchoyo, na uasherati ukaenea kila mahali. Watu hawakujizuia kutenda uhalifu wo wote ambao kwa huo wangeweza kujipatia mali au cheo. Majumba ya kifalme ya mapapa na maaskofu yalikuwa ni mahali pa kufanyia uasherati mchafu kabisa. Baadhi ya [mapapa] waliokuwa wakitawala walikuwa na hatia ya kutenda uhalifu [makosa ya jinai] wa kuchukiza mno hata watawala wa kidunia wakajaribu kuwaondoa katika utawala wakuu wale wa kanisa na kuwaona kama vile ni madubwana [majitu ya kutisha] maovu mno kuweza kuvumiliwa. Kwa karne nyingi hapakuwa na maendeleo yo yote kule Ulaya katika elimu, sanaa, au ustaarabu. Kupooza huko kimaadili na kiakili kulikuwa kumeuangukia Ulimwengu ule wa Kikristo.

Wanamatengenezo ya Kanisa Wapinga

Ukosefu wa maarifa ya kulijua Neno la Mungu uliuruhusu Upapa kuitawala dunia katika kipindi kile cha Zama za Giza. Karibu na mwisho wa kipindi kile, ufahamu wa Neno la Mungu ulipoanza kujidhihirisha, watu wakaanza kuyapinga mafundisho ya uongo yaliyozagaa wakati ule. Wanamatengenezo wale wa Kiprotestanti wakazitupilia mbali pingu zilizokuwa zimewafunga za mafundisho yale ya uongo na ushirikina, na kuanza kuiacha nuru ya Neno la Mungu ipate kuangaza. Watu hao walipewa cheo cha Waprotestanti, kwa sababu, kwa kadiri wao walivyoielewa kweli ya Neno la Mungu, waliona ya kwamba ni lazima wapinge na kuyakataa mafundisho ya uongo yaliyotolewa na Ukatoliki endapo wao wangekuwa ni wakweli kwa Mungu. Mara moja tena katika historia ya sayari hii maarifa ya kulijua Neno la Mungu yamekwisha kusahauliwa. Linganisha uelewa waliokuwa nao wale Wanamatengenezo ya Kanisa kuhusiana na Upapa na itikadi za kizazi hiki cha sasa.

Upapa Washutumiwa

Martini Lutheri alisema, "Mimi najua kwamba papa ndiye Mpinga Kristo, na ya kwamba jimbo lake [la Vatikani] ni la Shetani mwenyewe. Upapa ni mwindaji ajulikanaye na watu wote, kwa amri inayotolewa na Askofu wa Roma [Papa], kwa kusudi la kuwaponda-ponda na kuwaangamiza watu."

Charles Spurgeon [Spajoni] alisema hivi, "Yatupasa kuwaonya kwa ujasiri unaotumia busara wale wanaoelekea kwenye mafundisho ya uongo ya Roma; ni lazima tuwaambie mambo ya giza yanayofanywa na huo Upapa."

Yohana Noksi (John Knox) alisema kwamba papa alikuwa "ndiye Mpinga Kristo hasa."

Yohana Weslii (John Wesley) alisema hivi kuhusu Upapa, "Kwa maana ile yenye mkazo, yeye ndiye yule Mtu wa Dhambi (Man of Sin), kwa vile anazidisha kila aina ya dhambi kupita kiwango chake."

Yohana Kalvini (John Calvin) alisema, "Sisi tunamwita Mpinga Kristo huyo Askofu [Papa] wa Roma."

Waprotestanti Wasahau Yaliyopita

Hivi leo wazao wa wafiadini wale waaminifu wamesahau kwa nini wao wanajiita Waprotestanti. Hebu tafakari haya yafuatayo:

"Wakati umefika kwa Waprotestanti kumwendea mchungaji wao (papa) na kusema, 'Tunapaswa kufanya nini ili turudi nyumbani kwako?'" Dk. Robert Schuller, *Los Angeles Herald Examiner*, Sept. 19, 1987.

"Viongozi wa Makanisa ya Kiprotestanti ya Amerika pamoja na wale wa Makanisa ya Mashariki ya Kiothodoksi waliokuwa wakikutana na Papa Yohane Paulo II siku ya Ijumaa walisifia mjadala wao wa kwanza uliowawakilisha karibu wote kuwa ulikuwa ni tukio muhimu katika njia ya kufikia umoj a wa kuridhisha zaidi…. Mchungaji Paulo A. Crow (Mdogo), wa Indianapolisi, afisa wa ekumenio wa Kanisa la Kikristo (Wanafunzi wa Kristo), aliita kuwa ni 'siku mpya katika ekumenio' ikifungua mlango kwa siku za mbele ambazo katika hizo Mungu anatuvuta sisi kuwa pamoja.'" *The Montgomery Advertiser*, Sept. 12, 1987.

"Endapo Ukatoliki utazidi kuwa Ukatoliki zaidi kwa siku za usoni, jambo ambalo mimi natazamia kutokea chini ya papa wa sasa, basi, tofauti za kitheolojia zilizopo zitakuwa dhahiri zaidi, lakini ushirikiano wetu pamoja na Wakatoliki dhidi ya utamaduni wa kidunia unaweza kuwa na kina kirefu zaidi. Mimi, kwa upande wangu, niko tayari kujiunga nao." David Wells, *Eternity Magazine*, Sept. 1987.

"Mafundisho ya Kiprotestanti na Kikatoliki yenye haiba kubwa [mvuto mkubwa] juu ya maisha ya Kikristo yanalandana kabisa kwa maana yake yote pamoja na makusudi yake. Je, hilo si jambo la maana kwa Mkristo kwa siku zake za usoni?" J. J. Packer, *Christianity Today*, Juni 22, 1992.

Uprotestanti umesahau mizizi yake. Ulianzishwa kwa madhumuni ya kuyapinga na kuyashutumu mafundisho ya uongo ya Roma. Sasa uko tayari kuyakumbatia. Basi, kwa vile ulimwengu wote uko ukingoni mwa uvamizi wa mwisho kutoka Roma, adui wale wa zamani wanaungana pamoja. Ulimwengu wa Kiprotestanti umesahau kwamba umehusika katika kupigana vita ile ya milele, na kwa sababu ya kudharau maarifa hayo kwa hiari yao, basi, wamekabiliwa na maangamizi.

Sheria na Amani Ndiyo Hoja Hasa

Tangu mwanzo wa pambano hilo kuu kule mbinguni limekuwa ni kusudi la Shetani kuivunjilia mbali Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Ilikuwa ni kwa kusudi la kutekeleza jambo hilo yeye aliingia katika maasi yake dhidi ya Muumbaji wake, na ingawa alitupwa chini kutoka mbinguni, yeye ameendelea na vita ile ile juu ya dunia hii. Kuwadanganya watu, na kwa njia hiyo kuwashawishi kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ni lengo ambalo amelifuatilia kwa uthabiti sana. Endapo hilo litatekelezwa kwa kuitupa kando sheria yote kabisa, au kwa kuikataa katakata mojawapo ya amri zake [kumi], hatimaye matokeo yatakuwa ni yale yale. Anayekosea "katika neno [amri] moja," anaonyesha dharau yake juu ya Sheria nzima [Amri zote Kumi]; anakuwa "amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10.

Katika jitihada ya Shetani ya kuonyesha dharau yake juu ya amri [kumi] za Mungu, Shetani ameyapotoa mafundisho ya dini yatokayo katika Biblia, na kwa njia hiyo mafrundisho potofu yameingizwa katika imani ya maelfu ya wale wanaojidai kwamba wanayasadiki Maandiko hayo. Pambano kuu la mwisho kati ya kweli na uongo ni jitihada ya mwisho tu ya pambano hilo lililochukua muda mrefu sana dhidi ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Katika vita hiyo sisi sasa tunaingia - ni vita kati ya sheria za wanadamu na amri [kumi] za Yehova, kati ya dini ya Biblia na dini iliyojengwa juu ya hadithi za uongo na mapokeo.

Ukafiri umezagaa kote kwa kiwango cha kuogofya sana, si katika ulimwengu peke yake, bali ndani ya kanisa. Wengi wamekuja kuyakataa katakata mafundisho ya dini ambayo ni nguzo hasa za imani ya Kikristo. Mambo makuu ya kweli yahusuyo uumbaji kama yalivyoelezwa na waandishi wale waliovuviwa, anguko la mwanadamu, upatanisho, na umilele wa Sheria ya Mungu [Amri Kumi], yanakataliwa kabisa, ama yote, ama kwa sehemu yake, na sehemu kubwa ya Ulimwengu huu ujiitao wa Kikristo…. Wachungaji wengi wanawafundisha watu wao, wakisema kwamba Sheria ya Mungu [Amri Kumi] imebadilishwa, au imefutiliwa mbali; na wale wanaoyaona matakwa yake kuwa bado yana nguvu, kwamba yanapaswa kutiiwa neno kwa neno, hufikiriwa kuwa wanastahili tu kudhihakiwa na kudharauliwa.

Mafundisho ya Dini ni Ibada ya Sanamu

Kwa kuikataa ile kweli, watu humkataa Mwasisi wake. Kwa kuikanyaga Sheria ya Mungu [Amri Kumi] chini ya miguu yao, wanaikataa mamlaka ya huyo Mtoa-Sheria [Mtoa-Amri Kumi]. Ni rahisi kutengeneza sanamu ya mafundisho ya uongo pamoja na nadharia zake kama ilivyo rahisi kuchonga sanamu ya mti au jiwe. Kwa kuzielezea vibaya sifa za tabia yake Mungu, Shetani anawashawishi watu kumfikiria katika tabia ya uongo [isiyo yake]. Kwa wengi, sanamu ya falsafa imetawazwa kwenye kiti cha enzi mahali pa Yehova; wakati Mungu yule aliye hai, kama anavyofunuliwa katika neno lake, katika Kristo, na katika kazi zake za uumbaji, anaabudiwa na wachache tu. Maelfu wanayafanya maumbile [viumbe vya asili] kuwa ndiye mungu, huku wakimkana Mungu yule wa maumbile hayo. Ingawa ni katika mfumo tofauti, ibada hiyo ya sanamu imo katika Ulimwengu wa Kikristo leo kama ilivyokuwamo miongoni mwa Israeli ya kale katika siku zile za Eliya. Mungu wa wengi wanaojidai kuwa wana hekima, mungu wa wanafalsafa, watunzi wa mashairi, wanasiasa, waandishi wa habari - yaani, mungu wa jamii ile yenye malezi bora, kulingana na mtindo wa kisasa, ambao umo katika vyuo, na vyuo vikuu, na hata katika baadhi ya taasisi za kitheolojia - yu bora kidogo kuliko Baali, yaani, yule mungu-jua wa Wafoenike.

Hakuna fundisho la uongo lililopokewa na Ulimwengu wa Kikristo linaloigonga kwa ushupavu zaidi ile mamlaka ya Mbinguni, hakuna linalopingana moja kwa moja na sababu za busara zinazomwongoza mtu, hakuna lililo na athari kubwa zaidi kama fundisho la siku hizi, linaloenea kote kwa haraka mno, lisemalo kwamba Sheria ya Mungu [Amri Kumi] haiwafungi tena wanadamu…. Hebu na tuseme kwamba wachungaji hao maarufu wangefundisha hadharani kwamba amri zile zinazoiongoza nchi yao na kuzilinda haki za raia zake zilikuwa haziwafungi tena - kwamba zilikuwa zinawanyima uhuru wananchi, na kwa hiyo zilikuwa hazipaswi kutiiwa; je! ni kwa muda gani watu kama hao wangeweza kuvumiliwa katika mimbara zao? Lakini je! hivi ni kosa baya sana kutozijali sheria za serikali na za mataifa kuliko kuzikanyaga chini ya miguu yao amri zile [kumi] za Mungu ambazo ndizo msingi wa serikali zote?

Dhambi Haiwi Dhambi Tena

Po pote pale zinapokataliwa amri [kumi] za Mungu, dhambi inakoma kuonekana kwao kama ni dhambi, au haki kuweza kutamaniwa nao. Wale wanaokataa katakata kuitii serikali ya Mungu hawafai kabisa kujitawala wenyewe. Kwa njia ya mafundisho yao yenye madhara, roho ya kutotii inapandikizwa ndani ya mioyo ya watoto na vijana, ambao kwa kawaida hukosa subira wanapodhibitiwa; ndipo inatokea jamii iliyojaa uhalifu na uasherati. Wakati wao wanapowadhihaki wale walio wepesi kuyatii matakwa ya Mungu [Amri Kumi], watu wengi huyakubali madanganyo hayo ya Shetani. Wanajiachia katika tamaa zao za mwili na kutenda matendo ya dhambi ambayo yamepata kusababisha hukumu [za Mungu] kushuka chini juu ya washenzi [wapagani].

Jamii Yaparaganyika

Tayari fundisho la dini lisemalo kwamba watu wanawekwa huru ili wasitii matakwa ya Mungu [Amri Kumi za Mungu] limekwisha kuhafifisha nguvu ya uwajibikaji wao kimaadili na kufungua milango ya gharika ya maovu juu ya ulimwengu huu. Maasi, uasherati, na ufisadi hutufagia kama wimbi linalotushinda nguvu. Katika familia zetu, Shetani yuko kazini. Bendera yake hupepea, hata katika nyumba zile zinazojiita za Kikristo. Kuna wivu, kuwawazia wengine mabaya, unafiki, mafarakano, kushindana, magomvi, kuliacha tumaini lile takatifu, kujifurahisha katika tamaa mbaya za mwili. Mfumo mzima wa kanuni za dini pamoja na mafundisho yake, ambao ungejenga msingi na jukwaa la maisha ya kijamii, unaonekana kama jengo kubwa linalotikisika na lililo tayari kuanguka chini na kuwa magofu. Waovu kupindukia, wakitupwa gerezani kwa makosa yao, mara nyingi wanafanywa kuwa ni watu wa kupewa zawadi na kuwaangalia kana kwamba walikuwa wamepata cheo cha heshima kinachostahili kuonewa wivu. Habari zao zinatangazwa sana mbele ya watu kuhusu tabia zao na uhalifu wao walioufanya. Magazeti hutangaza maelezo ya kinagaubaga kuhusu uovu wao, hivyo huanza kuwafundisha wengine kufanya matendo yale ya udanganyifu, uporaji, na mauaji; naye Shetani hushangilia sana kufanikiwa kwa mbinu zake za kishetani. Kupenda maovu kiasi cha kurukwa na akili, kutojizuia kuuondoa uhai wa wengine, kuongezeka kwa namna ya kutisha kwa ulevi na maovu ya kila namna na ya kila kiwango, mambo hayo yangewashtua wale wote wanaomcha Mungu ili wapate kujiuliza ni kitu gani hasa kinaweza kufanywa kulizuia wimbi hilo la maovu.

Maandiko Sasa Yakataliwa

Uovu na giza la kiroho lililoenea kote chini ya Roma ilipokuwa imeshika hatamu za utawala wa dunia vilikuwa ni matokeo yasiyoepukika yaliyoletwa naye kwa kuyazuia Maandiko; lakini basi, ni wapi katika kizazi hiki cha uhuru wa dini panapoweza kupatikana chimbuko la ukafiri huu uliozagaa mahali pengi, pamoja na kuikataa Sheria ya Mungu [Amri Kumi], na ufisadi [rushwa] uliokuja kama matokeo yake, chini ya mng'aro huu kamili wa nuru ya Injili? Sasa kwa vile Shetani hawezi tena kuudhibiti ulimwengu mzima kwa kuyazuia Maandiko, basi, yeye anatumia njia nyinginezo kutimiza kusudi lake lile lile. Kuharibu imani ya watu katika Biblia hutimiza kusudi lake sawasawa kama kuiharibu kabisa Biblia yenyewe. Kwa kuanzisha imani ile isemayo kwamba Sheria ya Mungu [Amri Kumi] haiwafungi watu, kwa ufanisi amewaongoza watu kuivunja kana kwamba walikuwa hawazijui amri zake [kumi]. Na kwa wakati huu wa sasa, kama katika zama zile za kale, amefanya kazi yake kupitia ndani ya kanisa ili kuziendeleza mbinu zake hizo [2 Kor. 11:13-15; Yer. 14:14-16; Mt. 7:21-23; 24:24]. Mashirika ya dini ya siku hizi yamekataa katakata kuzisikiliza kweli zile zisizopendwa na watu wengi ambazo zimefunuliwa wazi katika Maandiko, na ili kupambana nazo wametumia tafsiri zao na kuwa na misimamo yao ambayo imepanda mbegu za kulishuku Neno la Mungu zilizotawanywa kila mahali.

Wakiling'ang'ania fundisho la uongo la papa lisemalo kwamba mwanadamu ana roho isiyokufa kamwe na kwamba akifa bado anaweza kuwa na fahamu zake za kujua mambo, wameikataa kinga pekee dhidi ya madanganyo ya imani ya mizimu. Fundisho la mateso yanayoendelea milele na milele limewafanya wengi wasiweze kuiamini Biblia. Na wakati madai ya amri ile ya nne [Sabato/Jumamosi - Kut. 20:8-11] yanaposisitizwa juu ya watu, wanagundua kwamba utunzaji wa Sabato ile ya siku ya saba [Jumamosi] ni amri; na kama njia yao ya pekee ya kujiweka huru wenyewe mbali na jukumu hilo wasilotaka kulitenda, waalimu wengi wanaopendwa sana na watu wengi wanawatangazia kwamba Sheria ya Mungu [Amri Kumi] haiwafungi tena watu [yaani, hawawajibiki kuitunza]. Kwa njia hiyo wanaitupilia mbali Sheria hiyo pamoja na Sabato [Jumamosi] yake. Kazi ya kufanya Matengenezo ya Sabato [kuwarudisha watu wote katika utunzaji wa Sabato] inapozidi kuenea mahali pengi, huko kuikataa hiyo Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ili kuyakwepa madai ya amri ile ya nne [Sabato/Jumamosi] kutakuwa karibu sana kumeenea ulimwenguni kote.

Zama za Giza Zarudiwa

Mbinu ya Shetani katika pambano hili la mwisho ni ile ile aliyoitumia katika kulianzisha pambano hili kuu kule mbinguni. Alidai kwamba yeye alikuwa anajaribu kuimarisha nguvu ya serikali ya Mungu, wakati kisirisiri anatumia juhudi yake yote katika kuhakikisha kwamba inapinduliwa kabisa. Na kazi iyo hiyo [ya mapinduzi] aliyokuwa akijitahidi kuikamilisha kwa njia hiyo, akawatupia lawama malaika wale waaminifu. Mbinu iyo hiyo ya udanganyifu imetia waa katika historia ya Kanisa la Roma. Limejidai kutenda kazi yake kama liko Badala ya Mungu, wakati uo huo limejitahidi sana kujiinua juu ya Mungu na kuibadili Sheria yake [Amri Kumi - Dan. 7:25; 2 The. 2:3,4]. Chini ya utawala wa Roma, wale walioteswa hadi kuuawa kwa ajili ya uaminifu wao kwa ile injili, walishutumiwa kama watenda maovu; walitangazwa kwamba walikuwa wanashirikiana na Shetani; na kila njia iliyowezekana ilitumika ili kuwafunika na aibu, yaani, kuwafanya waonekane mbele ya macho ya watu na hata machoni pao wenyewe kama ni wahalifu wabaya kupindukia. Hivyo ndivyo itakavyokuwa sasa. Wakati Shetani anajitahidi sana kuwaangamiza wale wanaoiheshimu Sheria ya Mungu [Amri Kumi - Kut. 20:3-17; Ufu. 12:17; Yn. 8:44]; atafanya wapate kushtakiwa kama wavunjaji wa sheria, yaani, kama ni watu wanaomwaibisha Mungu na kuleta hukumu zake juu ya dunia hii.

Kulazimisha kwa Kutumia Ukatili

Mungu hailazimishi kamwe nia au dhamiri ya mtu; lakini juhudi ya Shetani ya kudumu - yaani, ya kutaka kuwadhibiti wale asioweza kuwashawishi kwa njia nyingine yo yote - ni kuwalazimisha kwa kutumia nguvu iliyojaa ukatili mwingi. Kwa kuwatia hofu hiyo au kutumia nguvu anajitahidi sana kuzitawala dhamiri zao na kuwafanya wamsujudie yeye mwenyewe [Ufu. 13:4,7,8]. Kutimiza hayo, anafanya kazi yake kupitia kwa wote wawili, yaani, kupitia kwa wenye mamlaka wa kidini na wale wa kiserikali, akiwasukuma kutunga sheria za kibinadamu zinazoipiga vita Sheria ya Mungu [Amri Kumi].

Wale wanaoiheshimu Sabato ya Biblia [Jumamosi] watashutumiwa kama maadui wa sheria na amani ya nchi, kama wakiukaji [wavunjaji] wa vizuio vya kimaadili katika jamii, wanaosababisha maasi dhidi ya serikali na kuleta ufisadi, na kuzileta hukumu za Mungu hapa chini juu ya dunia hii. Kukataa kwao kunakotokana na dhamiri zao, kutatangazwa kuwa ni kiburi, ukaidi, na dharau kwa wenye mamlaka. Watashtakiwa kuwa ni waasi dhidi ya serikali yao. Wachungaji wanaokana kuwa watu hawawajibiki kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] watahubiri toka katika mimbara zao juu ya wajibu wa kuwatii wenye mamlaka katika serikali za kiraia kuwa ndiyo amri ya Mungu. Katika kumbi za Mabunge na mahakama za sheria, wale wanaozishika amri [kumi] wataelezwa vibaya na kuhukumiwa [Mt. 10:17-23]. Picha ya uongo itawekwa juu ya maneno yao waliyosema; picha mbaya mno itawekwa juu ya makusudi yao kwa mambo yale wanayoyatenda.

Wale wanaoiheshimu Sabato ya Biblia watashutumiwa kama maadui wa sheria na amani ya nchi.

Kubadilishana Nuru kwa Giza

Makanisa ya Kiprotestanti yanapozikataa hoja hizo za Maandiko zinazoeleweka wazi ambazo zinaitetea Sheria ya Mungu [Amri Kumi], watatamani sana kuwanyamazisha wale ambao hawawezi kuipindua imani yao kwa kutumia Biblia. Ingawa wao wanajifanya wenyewe kuwa vipofu ili wasiweze kuuona ukweli huo [Eze. 22:26-29], hivi sasa wanaichagua njia ile itakayowafikisha katika kuwatesa wale ambao, kutokana na vile dhamiri zao zinavyowakataza, wanakataa kufanya kile ambacho Ulimwengu uliobaki wa Kikristo unafanya, na kukataa kuyakubali yale madai ya sabato ya papa [Jumapili].

Wanyimwa Uhuru wa Dhamiri

Viongozi wakuu wa kanisa na serikali wataungana pamoja ili kuwahonga, kuwashawishi, au kuwalazimisha kwa kutumia nguvu watu wa tabaka zote ili wapate kuiheshimu Jumapili. Kukosekana kwa idhini ya Mungu kutazibwa kwa kutunga sheria kali za ukandamizaji Bungeni. Rushwa katika siasa inaharibu kuipenda haki na kuijali ile kweli; na hata katika Amerika huru, watawala na watunga sheria [wabunge], ili kujipatia upendeleo kwa wananchi, watayakubali madai yale yanayopendwa na watu wengi kwamba iwepo sheria inayolazimisha utunzaji wa Jumapili. Uhuru wa dhamiri, ambao umewagharimu watu mno kwa kujitolea kwao mhanga, hautaheshimiwa tena. Katika pambano hilo lililo karibu sana kutokea tutajionea wenyewe maneno haya ya nabii yakitimia kwa vitendo: "Joka [Shetani] akamkasirikia yule mwanamke [kanisa safi], akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia [wafuasi wake wa mwisho], wazishikao amri [kumi] za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu" [Roho ya Unabii - Ufu. 19:10]. Ufunuo 12:17.

Uhuru wa dhamiri,
ambao umewagharimu
watu mno kwa kujitolea
kwao mhanga,
hautaheshimiwa tena.

Kuifafanua Mifano Iliyotumika

Kuwatofautisha na wale wazishikao amri [kumi] za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, malaika yule wa tatu anasonda kidole chake kwenye kundi jingine, ambalo dhidi ya makosa yao onyo hili zito na la kutisha linatamkwa: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa (alama) katika kipaji cha uso wake [katika fikra zake], au katika mkono [uwajibikaji] wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu [Mapigo 7 ya Ufu. 16; 15:1]. Ufunuo 14:9,10. Tafsiri sahihi ya mifano hiyo iliyotumika hapo ni lazima ili kuweza kuuelewa ujumbe huo. Ni kitu gani kinachowakilishwa na mnyama, sanamu ya mnyama, chapa (alama) ya mnyama?

Joka

Mkondo wa unabii ambao mifano hiyo inapatikana ndani yake unaanzia na Ufunuo 12 na yule joka aliyejaribu kumwangamiza Kristo wakati wa kuzaliwa kwake. Joka huyo anasemekana kuwa ni Shetani (Ufunuo 12:9); yeye ndiye aliyemsukuma Herode kumwua Mwokozi. Lakini kibaraka mkubwa wa Shetani katika kufanya vita dhidi ya Kristo na watu wake katika kipindi kile cha karne zile za kwanza za Kipindi cha Kikristo ilikuwa ni ile Dola ya Roma, ambayo ndani yake upagani ulikuwa ndiyo dini yake iliyoenea kote. Hivyo, japokuwa kimsingi Joka anamwakilisha Shetani, kwa maana ile ya pili, huyo [Joka] ni ishara ya Roma ya Kipagani.

Mnyama Mfano wa Chui

Katika Sura ya 13 (fungu la 1 hadi la 10) anaelezwa mnyama [mfalme/ufalme - Dan. 7:17] mwingine, aliyekuwa "mfano wa chui," ambaye Joka huyo alimpa "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Mfano huo, kama walivyoamini Waprotestanti wengi sana, huwakilisha Upapa, ambao ulirithi nguvu na kiti cha enzi na uwezo uliokuwa umeshikiliwa kwanza na Dola ya Roma ya Kale. Kwa habari ya mnyama huyo mfano wa chui inatangazwa hivi: "Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu na makufuru…. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na [dhidi] watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa [fungu la 5 hadi la 7 KJV]. Unabii huo, ambao unalandana karibu sana na maelezo ya ile Pembe Ndogo ya Danieli 7, pasipo shaka lo lote unasonda kidole chake kwa Upapa.

"Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili" [fungu la 5]. Naye nabii asema hivi, "Nikaona kimoja cha vichwa vyake [watawala wake - Ufu. 17;9,10] kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti" [fungu la 3]. Na tena anasema hivi: "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga" [fungu la 10]. Miezi ile arobaini na miwili [miezi 42 x siku 30 = siku/miaka 1260] ni sawa na "nyakati na nusu wakati" [Ufu. 12:14; Dan. 7:25], yaani, sawa na miaka mitatu na nusu ya Danieli 7 [miaka 3 1/2 x siku 360 = siku/miaka 1260; siku 1 = mwaka 1 (Eze. 4:6)] - yaani, hicho ni kipindi ambacho mamlaka ya papa

ingewatesa watu wa Mungu. Kipindi hicho, kama ilivyoelezwa katika Sura zilizotangulia, kilianza na upapa uliposhika hatamu za utawala wa dunia (papal supremacy) katika mwaka ule wa 538 B.K., nacho kilikoma mwaka ule wa 1798 [1798-538 = miaka 1260]. Wakati ule papa [Piusi wa VI] alichukuliwa mateka na jeshi la Kifaransa [lililoongozwa na Jenerali Berthier], hapo ndipo mamlaka ile ya kipapa ilipotiwa jeraha lake la mauti [ilipoteza uwezo wake wa kuitawala dunia - Ufu. 17:18], tena likawa limetimizwa neno hili lililotabiriwa, "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka." Ufunuo 13:10.

"Kwa hiyo, kama Kanisa Katoliki pia kwamba linayo haki ya kutoyavumilia mafundisho ya dini yaliyo tofauti na yake, si hakikulishutumu likiitumia haki hiyo....Linaona kwamba kule kutoyavumilia mafundisho ya dini yaliyo tofauti na yake sio haki yake tu isiyoweza kupingwa, bali pia ni wajibu wake mtakatifu.... Kwa mujibu wa Warumi 8:11, mamlaka zile za kidunia zinayo haki ya kutoa adhabu, ya kifo, hasa kwa uhalifu mkubwa, kwa hiyo, 'wazushi hawapaswi kutengwa tu na kanisa, bali pia kuuawa kwa haki.'" *The Catholic Encyclopedia*, **toleo la 1911, gombo la 14, ukurasa 766,768.**

Amerika Katika Unabii

Mpaka hapo mfano mwingine unaletwa kwetu. Asema hivi huyo nabii: "Kisha nikaona mnyama [ufalme - Dan. 7:17] mwingine, akipanda juu katika nchi [mahali pasipokuwa na watu au walipo wachache tu]; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo." Fungu la 11. Mambo yote mawili, yaani, mwonekano wa mnyama huyo na jinsi alivyotoka huonyesha kwamba taifa linalowakilishwa naye halifanani na yale yaliyoelezwa katika mifano iliyotangulia. Falme zile kuu zilizoutawala ulimwengu huu zilionyeshwa kwa nabii Danieli kama wanyama wakatili wanaokamata mawindo [wanaoteka nyara], waliotokea wakati zile "pepo nne za mbinguni [vita] zili[po]vuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa." Danieli 7:2. Katika Ufunuo 17 malaika alifafanua kwamba maji (bahari) yale yaliwakilisha "jamaa na makutano na mataifa na lugha." Ufunuo 17:15. Pepo ni mfano wa vita. Pepo nne za mbinguni zilizovuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa huwakilisha matukio ya kutisha ya ushindi vitani na mapinduzi ambayo kwayo falme zile zilijitwalia mamlaka yake.

Akipanda Juu Katika Nchi

Lakini myama [ufalme] yule mwenye pembe kama mwana-kondoo alionekana "akipanda juu katika nchi." Ufunuo 13:11. Badala ya [ufalme ule] kuzipindua mamlaka zile nyingine ili kujiimarisha, taifa lililowakilishwa hivyo ni lazima litokee katika nchi isiyokaliwa na watu na kukua taratibu na kwa amani. Basi, lisingeweza kutokea miongoni mwa mataifa yanayopigana ya Ulimwengu ule wa Zamani [Ulaya] ambayo yana msongamano wa watu - yaani, lisingetokea katika bahari ile iliyochafuka ya "jamaa na makutano na mataifa na lugha." Ni lazima litafutwe katika Kontinenti la Magharibi.

Je, ni taifa gani la Ulimwengu Mpya [Amerika] lililokuwa likitokea na kujitwalia mamlaka yake, likitoa matumaini ya kuwa na nguvu na ukuu, na kuyavuta mawazo ya ulimwengu mzima? Matumizi ya mfano huo hayakaribishi hoja yo yote. Taifa moja, na moja tu, linatimiza maelezo yote ya unabii huo. Unasonda kidole chake bila kukosea kwa Marekani (U.S.A.). Tena na tena wazo hilo, karibu na kutumia maneno yale yale kabisa ya mwandishi huyo mtakatifu, limetumika bila kutambua na mnenaji na mwanahistoria aliyeeleza kutokea na kukua kwa taifa hilo. Mnyama [ufalme] yule alionekana "akipanda juu kutoka katika nchi;" na kufuatana na wafasiri, neno hili "kupanda juu" lililotumika hapo maana yake ikichukuliwa neno kwa neno ni "kukua au kuchipua kama mmea." Na, kama mlivyokwisha kuona, taifa hilo ni lazima litokee katika nchi ambayo haijapata kukaliwa na watu siku za nyuma. Mwandishi mmoja maarufu, akieleza kutokea kwa Marekani (U.S.), anazungumza juu ya "siri ya kupanda kwake

juu kutoka mahali pa ukiwa," tena anasema hivi: "Kama mbegu iliyo kimya tulikua na kuwa dola." - G. A. Townsend, *The New World Compared With the Old*, ukurasa 462. Jarida la Ulaya katika mwaka ule wa 1850 liliongelea juu ya Marekani (U.S.) kama dola ya ajabu ambayo ilikuwa "inajitokeza," "katikati ya ukimya wa nchi ile, na kuongezeka nguvu zake na fahari yake kila siku." - *The Dublin Nation*.

Zile "pembe mbili kama mwana-kondoo" zinawakilisha vizuri tabia ya serikali yetu, kama ilivyoelezwa katika kanuni zake za msingi mbili - Ujamhuri na Uprotestanti. "Kanuni hizo ndiyo siri ya uwezo na usitawi wake." Wale waliokuwa wa kwanza kupata kimbilio lao katika pwani zile za Amerika, walishangilia kwamba walikuwa wamefika katika nchi iliyokuwa huru mbali na madai ya majivuno makuu ya upapa na ukandamizaji wa utawala wa kifalme. Wakadhamiria kuanzisha serikali yao juu ya msingi mpana wa Uhuru wa Serikali na Uhuru wa Dini.

> **"Ukuta unaotenganisha kati ya Kanisa na Serikali ni usemi uliojengwa juu ya historia mbaya, usemi ambao umeonekana kuwa haufai kabisa kama mwongozo wa kuamua mambo. Kusema kweli ungepaswa kutupiliwa mbali kabisa. Chief Justica William Rehnquist,** *Time*, **Desemba 9, 1991.**
>
> **Hukumu iliyotolewa hivi karibuni na Mahakama Kuu ya Marekani "ilitangaza kwamba haki za kidini zinapogongana na mahitaji ya serikali ya kuwa na sheria za aina moja, mahakama hii itasimama upande wa serikali."** *Los Angeles Times*, **Aprili 18, 1990.**

Anena Kama Joka

Lakini yule mnyama [ufalme] mwenye pembe mbili kama mwana-kondoo "akanena kama Joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama [mfalme] yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudu mnyama [mfalme yule] wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona…. Akiwaambia [kidemokrasia] wale wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu ya [mfano wa] yule mnyama [mfalme], aliyekuwa na jeraha la mauti naye akaishi" [upapa]. Ufunuo 13:11-14.

Pembe zile mfano wa mwana-kondoo na sauti ile ya joka katika mfano huo huonyesha tofauti dhahiri iliyopo kati ya maneno linayosema na matendo ya taifa hilo lililowakilishwa kwa njia hiyo. Kule "kunena" kwa taifa hilo ni utendaji wa mamlaka yake ya kutunga sheria [Bunge] na mahakama. Kwa utendaji kama huo litasema uongo dhidi ya kanuni zile za uhuru na amani ambazo limezitoa kama msingi wa sera zake. Utabiri kwamba litanena "kama joka" na ku"tumia uwezo wote wa mnyama [mfalme] yule wa kwanza" hutabiri waziwazi juu ya kukuzwa kwa roho ile ya kutovumilia imani ya wengine na kuwatesa, ambayo ilidhihirishwa na mataifa yale yaliyowakilishwa na joka [Shetani] na mnyama [mfalme] yule mfano wa chui. Na usemi huo kwamba mnyama [ufalme] mwenye pembe mbili "aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama [mfalme] yule wa kwanza" [upapa] huonyesha kwamba mamlaka ya taifa hilo itatumika katika kulazimisha kisheria uadhimishaji wa aina fulani, tendo ambalo litakuwa ni kuusujudia huo Upapa.

Tendo kama hilo moja kwa moja litakuwa kinyume na kanuni za serikali hiyo, kinyume na taasisi zake za pekee zilizo huru, kinyume na maneno yake mazito yaliyo katika Tangazo la Uhuru, na kinyume na Katiba ya Nchi. Waasisi wa Taifa hilo kwa hekima walijitahidi sana kuweka kinga dhidi ya kuitumia mamlaka [serikali] ya kidunia kwa upande wa kanisa, pamoja na matokeo yake yasiyoepukika - yaani, kutovumilia imani ya wengine na kuwatesa. Katiba ya Nchi hiyo inaweka sharti kwamba "Bunge la Marekani (Congress) halitatunga sheria yo yote inayohusu dini, au kupiga marufuku uendeshaji huru wa dini hiyo," na ya kwamba "hakuna kipimo cho chote cha kidini kitakachotakiwa kama sifa ya kukalia cheo cho chote cha umma chenye amana katika nchi ya Marekani (U.S.). Ni kwa ukiukaji tu usio na haya wa kinga hizo zilizowekwa kwa ajili ya uhuru wa taifa hilo yanaweza kulazimishwa kisheria na mamlaka ya serikali maadhimisho yawayo yote ya kidini. Lakini mageuzi yaliyoletwa na kitendo kama hicho si makubwa kuliko ule mfano wenyewe. Ni yule mnyama [ufalme] mwenye pembe kama mwana-kondoo - ambaye kwa maneno yake ni safi, mpole, wala hana madhara yo yote - ambaye atanena kama joka.

Marekani Yabadilisha Katiba ya Nchi
-
Yaitungia Sheria Bungeni
Sabato ya Papa
-
Yanena Kama Joka

Sanamu ya Mnyama

"Akiwaambia wakaao juu ya nchi [akiwaomba kidemokrasia wananchi wa Marekani] wamfanyie sanamu [mfumo wa serikali unaofanana na ule wa] yule mnyama [mfalme papa]." Hapo unawakilishwa waziwazi mfumo wa serikali ambao mamlaka yake ya kutunga sheria [Bunge] inawawakilisha wananchi [demokrasia], ushahidi huo ni dhahiri kabisa kwamba Marekani (U.S.) ndilo taifa linalotajwa katika unabii huo.

Lakini, je! "sanamu ya mnyama" ni nini? Tena itaundwaje? Sanamu hiyo inaundwa na mnyama yule mwenye [ufalme ule wenye] pembe mbili [Marekani], tena ni sanamu *kwa* [ajili ya] huyo mnyama [mfalme papa]. Pia inaitwa sanamu *ya* mnyama [mfalme papa]. Basi, ili kujua jinsi sanamu hiyo ilivyo na jinsi itakavyoundwa ni lazima sisi tujifunze tabia halisi za yule mnyama [mfalme papa] mwenyewe - yaani, [tujifunze tabia za] Upapa.

Muungano wa Kanisa na Serikali

Kanisa lile la mwanzo lilipoingia katika ufisadi kwa kuiacha injili rahisi na kupokea taratibu za ibada ya kishenzi [kipagani] pamoja na desturi zake, lilimpoteza Roho na uweza wa Mungu; na ili lipate kuzitawala dhamiri za watu [liwazuie watu kumwabudu Mungu wanavyotaka], liliomba msaada kutoka kwa mamlaka [serikali] ya kidunia. Matokeo yake yakawa huo upapa, yaani, kanisa lililoitawala mamlaka ya serikali na kuitumia kuendeleza makusudi yake, hasa kwa ajili ya kuuadhibu "uzushi" [Roma inayaita mafundisho safi ya Biblia kuwa ni uzushi (uongo)]. Ili Marekani ipate kuiunda sanamu hiyo ya mnyama [mfumo huo wa utawala unaofanana na upapa, yaani, mtu mmoja kuvaa kofia mbili - dini na serikali], ni lazima mamlaka ile ya kidini [yaani, ya Uprotestanti wa Marekani] iitawale kabisa serikali ya kiraia kiasi kwamba mamlaka ya serikali itatumiwa pia na kanisa [la Kiprotestanti] kutimiza makusudi yake [kama vile papa alivyofanya].

Ulikuwa ni uasi ulioliongoza kanisa lile la kwanza [Roma] kuomba msaada kwa serikali ya kiraia, na jambo hilo lilitayarisha njia ya kuukuza upapa - yaani, yule mnyama [mfalme papa]. Alisema hivi yule Paulo: "Usipokuja" ule "ukengeufu [kuanguka kutoka katika ile kweli]; akafunuliwa [akafichuliwa] yule Mtu wa Dhambi (Man of Sin)" - 2 Wathesalonike 2:3. Kwa hiyo, uasi ndani ya kanisa [la Kiprotestanti la Marekani] utatayarisha njia ya kuundwa kwa Sanamu ya Mnyama [mfumo wa serikali ya Kiprotestanti ya Marekani unaofanana na ule wa upapa - mtu mmoja kuvaa kofia mbili].

Historia Yajirudia

Biblia inatangaza kwamba kabla ya marejeo yake Bwana patakuwa na hali ya kushuka katika mambo ya kidini kama ile iliyotokea katika karne zile za kwanza. "Siku za mwisho kutakuwako na nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wanaowadharau walio wema [KJV], wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake." 2 Timotheo 3:1-5. "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Shetani atatenda kwa "madanganhyo yote ya udhalimu." Ndipo wale wote ambao "hawakukubali kuipenda [kuishi kulingana na] ile kweli [Yn. 17:17; Zab. 119:142], wapate kuokolewa," wataachwa ili waipokee ile "nguvu ya upotevu, wauamini uongo [mafundisho potofu]." 2 Wathesalonike 2:9-11. Hali hiyo ya uovu itakapofikiwa, matokeo yale yale yatafuata kama vile yalivyokuwa katika karne zile za mwanzo.

Kuundwa kwa ile Sanamu

Makanisa makuu ya Marekani yakiungana katika vipengele kama hivyo vya mafundisho ya dini wanavyokubaliana navyo wote, yatakapoishawishi serikali [ya Marekani] kuzitungia sheria Bungeni amri zao na kuzipa msaada wa fedha [ruzuku] taasisi zao, hapo ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakapokuwa imeunda sanamu ya utawala ule msonge wa kidini wa Roma [Sanamu ya Mnyama], na matokeo yake yasiyoepukika yatakuwa ni kutoa adhabu kali kwa msaada wa serikali dhidi ya wale wasiokubaliana na mafundisho yao ya dini.

Alama ya Mnyama

Mnyama yule mwenye [ufalme ule wenye] pembe mbili "awafanya [awalazimisha] wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa (alama) katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa (alama) ile, yaani, jina la mnyama [mfalme] yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16,17. **Onyo** la Malaika yule wa Tatu ni hili: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama [mfalme papa] na sanamu yake [Uprotestanti Asi uliojiunga na Roma], na kuipokea chapa [alama] katika kipaji cha uso wake [katika fikra zake], au katika mkono [utendaji] wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu" [atapigwa na Mapigo yale 7 ya Ufunuo 16; 15:1]. Yule "Mnyama" [mfalme] aliyetajwa katika ujumbe huo, ambaye kumsujudu kutalazimishwa na mnyama yule mwenye pembe mbili [Marekani], ni wa kwanza, au ni yule mnyama mfano wa chui wa Ufunuo 13 - yaani, ni Upapa. "Sanamu ya Mnyama" huuwakilisha mfumo ule wa Uprotestanti Asi utakaojitokeza wakati ule makanisa ya Kiprotestanti yatakapoomba msaada toka kwa mamlaka ya serikali kwa ajili ya kuyatungia sheria Bungeni mafundisho yao ya dini. "Alama (Chapa) ya Mnyama [mfalme papa]" bado haijafafanuliwa.

Ibada Yatofautishwa

Baada ya onyo hilo dhidi ya kumsujudu huyo mnyama [mfalme papa] na sanamu yake [Uprotestanti Ulioasi mafundisho ya Biblia], unabii huo unatangaza hivi: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri [kumi] za Mungu, na imani ya Yesu" [Ufu. 14:12]. Kwa kuwa wale wazishikao amri [kumi] za Mungu wanatofautishwa kwa njia hiyo na wale wanaomsujudu mnyama [mfalme papa] na sanamu yake [Uprotestanti Asi] na kupokea chapa (alama) yake, basi, inafuata ya kwamba kule kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa upande mmoja, na kuivunja, kwa upande ule wa pili, **kutaweka tofauti kati ya wale wanaomsujudu Mungu na wale wanaomsujudu mnyama [mfalme papa - 2 The. 2:4]**.

"Lengo la mwisho la Ekumenio, kama wanavyolifahamu Wakatoliki, ni umoja katika imani, ibada, na katika kuitambua mamlaka kuu kuliko zote ya kiroho aliyo nayo askofu [Papa] wa Roma." Kasisi J. Cornnell.

Tabia ya Huyo Mnyama

Tabia ya pekee ya mnyama [mfalme] huyo, na kwa hiyo, ya sanamu yake, ni ile ya **kuzivunja amri [kumi - Yak. 2:10-12] za Mungu**. Asema hivi Danieli kuhusu Pembe ile Ndogo [Mfalme yule - Dan. 7:24], yaani, Upapa: "Naye **ataazimu kubadili majira na Sheria [Amri Kumi]**." Danieli 7:25. Naye Paulo aliipa jina mamlaka iyo hiyo [ya papa] kuwa ni "**mtu wa dhambi**" (man of sin), ambaye alitarajiwa kujiinua mwenyewe juu ya Mungu [2 The. 2:4]. Unabii huo mmoja unaukamilisha ule mwingine. Ni kwa njia peke yake ya kuibadili Sheria ya Mungu [Amri Kumi] upapa ungeweza kujitukuza [kujiweka] wenyewe juu ya Mungu; mtu ye yote ambaye, hali akijua, ataitunza Sheria [Amri Kumi] hiyo iliyobadilishwa, atakuwa anaipa heshima kubwa mno isiyo na kifani mamlaka hiyo [ya papa] ambayo ilifanya badiliko hilo. Tendo kama hilo la kutoa utii kwa sheria zile zilizowekwa na papa lingekuwa ni **alama (chapa) ya utii kwa papa** badala ya kumtii Mungu.

Hapo badiliko la makusudi kabisa, lililodhamiriwa linaelezwa: "Naye ataazimu [atanuia] kubadili majira [siku ya ibada] na Sheria [Amri Kumi]." Badiliko lililofanyika katika amri ile ya nne [Kut. 20:8-11] hutimiza unabii huo kabisa. Hapo mamlaka hiyo ya papa inajiweka yenyewe waziwazi juu ya Mungu.

Utakatifu wa Jumamosi

Wakati wale wanaomsujudu Mungu watatambulikana kwa njia ya pekee kwa kuitunza amri ile ya nne [Kut. 20:8-11; 31:16,17; Eze. 20:12,20], - kwa kuwa hiyo ndiyo ishara ya uweza wake wa uumbaji, tena ni ushuhuda wa madai yake juu ya mwanadamu ili amche na kumsujudu yeye, - wale wanaomsujudu yule mnyama [mfalme papa] watatambulikana kwa juhudi zao za kuivunjilia mbali kumbukumbu hiyo ya Muumbaji, wakiitukuza siku ile [ya Jumapili] iliyowekwa na Roma. Ilikuwa ni kwa ajili ya hiyo Jumapili upapa, kwa mara yake ya kwanza, ulitoa madai yake yaliyojaa majivuno makuu; na utumiaji wake wa mamlaka ya serikali kwa mara ya kwanza ulikuwa na madhumuni ya kulazimisha kwa kutumia nguvu za dola uadhimishaji wa Jumapili kama "Siku ya Bwana." Lakini Biblia inasonda kidole chake kwenye siku ile ya saba [Jumamosi], wala sio kwenye ile ya kwanza [Jumapili] kama Siku ya Bwana [Ufu. 1:10; Mt. 12:8,12]. Alisema hivi Kristo: "Basi Mwana wa Adamu [Kristo] ndiye **Bwana (Yehova) wa Sabato pia**." Amri ile ya nne hutangaza hivi: "Siku ya saba [Jumamosi] ni Sabato ya BWANA (YEHOVA)" [sio ya Wayahudi kama wasemavyo viongozi wa dini - Kut. 20:10]. Na kupitia kwa nabii Isaya Bwana anaiita siku hiyo: "Siku ya utakatifu wangu." Marko 2:28; Isaya 58:13.

Wakatoliki wa Roma wanakiri kwamba badiliko hilo la Sabato [Jumamosi] lilifanywa na kanisa lao, nao wanatangaza kwamba Waprotestanti kwa njia ya kuiadhimisha Jumapili wanaitambua mamlaka yao [Roma]…. Kama ishara ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, waandishi wengi ambao ni wafuasi

wa papa wanalitaja "tendo lile hasa la kuibadili Sabato [Jumamosi] kuwa Jumapili, yaani, tendo lile wanalolikubali Waprotestanti;… kwa sababu kwa kuitunza Jumapili, wanaukubali uwezo wa kanisa wa kuamuru sikukuu, na kuwaamuru wawe chini ya dhambi." - Henry Tuberville, *An Abridgment of the Christian Doctrine*, ukurasa 58. Maana yake ni nini, basi, hilo badiliko la Sabato [Jumamosi], kama sio ile *ishara* au *alama* ya mamlaka ya Kanisa la Roma - yaani, "*Alama (Chapa) ya Mnyama*"[Alama ya Mfalme Papa

"**Jumapili ni alama ya mamlaka yetu. Kanisa ni zaidi ya Biblia, na huko kuhamishwa kwa utunzaji wa Sabato ndio ushahidi wa jambo hilo."** *The Catholic Record*, **London, Ontario, Septemba 1, 1923.**

"Utunzaji wa Jumapili unaofanywa na Waprotestanti ni kuisujudu mamlaka ya Kanisa [Katoliki], wakiwa wanajipinga wenyewe." Monsignor Segur, *Plain Talk About Protestantism of Today*, ukurasa 213.

Kuikataa Biblia

Kanisa hilo la Roma halijalitupilia mbali dai lake la ukuu kuliko wote; na ulimwengu pamoja na makanisa ya Kiprotestanti wanapoikubali sabato iliyowekwa nalo [Jumapili], na kuikataa Sabato ya Biblia [Jumamosi], wanalikubali dai hilo [la kwamba papa ni mkuu kuliko wote]. Wanaweza kutoa madai yatokanayo na mapokeo pamoja na yale ya Mababa kwa badiliko hilo; lakini kwa kufanya hivyo wanaipuuzia kanuni ile ile hasa ambayo inawatenga mbali na Roma - isemayo kwamba, **Biblia, na Biblia peke yake**, hiyo ndiyo dini ya Waprotestanti." Mfuasi wa papa anaweza kuwaona [hao Waprotestanti] kuwa wanajidanganya wenyewe, kwa makusudi mazima wakifumba macho yao wasiuone ulivyo ukweli wa suala hilo [Eze. 22:26]. Tapo [kundi] lile linalotaka utunzaji wa Jumapili ulazimishwe kisheria, kadiri linavyozidi kupata upendeleo [machoni pa watu wengi], [mfuasi huyo wa papa] anashangilia, akiwa na hakika kuwa hatimaye [Jumapili hiyo] itauleta Ulimwengu wote wa Kiprotestanti chini ya bendera ya Roma.

Kumsujudu Mnyama

Lakini, basi, Wakristo wale wa vizazi vilivyopita waliitunza Jumapili wakidhani kwamba kwa kufanya vile walikuwa wanaitunza Sabato ile ya Biblia; tena hata sasa **wamo Wakristo wa kweli katika kila kanisa**, bila kuibagua jumuia ya Kikatoliki ya Roma, ambao kwa unyofu wao wa moyo wanaamini kwamba Jumapili ndiyo ile Sabato iliyowekwa na Mungu. Mungu analikubali kusudi lao litokanalo na unyofu wao wa moyo na uaminifu wao mbele zake. Lakini utunzaji huo wa Jumapili **utakapolazimishwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge, na ulimwengu wote utakapokuwa umepewa mwanga kuhusu Sabato ya kweli inayowafunga watu wote**, hapo ndipo ye yote yule atakayeivunja amri hiyo ya Mungu, ili kuitii amri ile isiyokuwa na mamlaka ya juu kuliko yale ya Roma, kwa njia hiyo atakuwa anaiheshimu Roma kuliko Mungu. **Atakuwa anaisujudu Roma** pamoja na mamlaka ile inayoitungia [Jumapili] sheria Bungeni ili kulazimisha [utunzaji wa] siku ile iliyowekwa na Roma. Mtu huyo anamsujudu mnyama [mfalme papa] na sanamu yake [Uprotestanti Asi]. Wakati ule wanadamu watakapoikataa katakata siku ile aliyoitangaza Mungu kwamba ni ishara ya mamlaka yake, na mahali pake kuiheshimu ile iliyochaguliwa na Roma kama ishara ya ukuu wake usio na kifani, kwa njia hiyo **wataipokea alama ya utii wao kwa Roma** - yaani, watapokea ile "**Alama (Chapa) ya Mnyama**" [Alama ya Mfalme Papa].

Tena jambo hilo halitakuwa hivyo mpaka suala hilo litakapokuwa limewekwa mbele ya watu wote kwa wazi, nao watafikishwa mahali pa **kuchagua kati ya Amri [Kumi] za Mungu na amri za wanadamu**, ndipo wale watakaoendelea kuzivunja amri hizo [za Mungu] watakapopokea "**Alama ya Mnyama**."

Tishio la Kuogofya

Tishio la kuogofya mno lililopata kunenwa dhidi ya wanadamu wenye maisha mafupi linapatikana katika Ujumbe wa Malaika yule wa Tatu. Hiyo inaweza kuwa ni dhambi ya kuogofya mno ambayo inafanya ghadhabu ya Mungu isiyochanganyika na rehema yake kushuka chini toka mbinguni. Watu hawapaswi kuachwa gizani kuhusu jambo hilo la maana; onyo dhidi ya dhambi hiyo linapaswa kutolewa kwa ulimwengu mzima kabla hukumu hizo za Mungu hazijapatilizwa, **ili wote wapate kujua kwa nini watapaswa kuteswa kwa hizo hukumu, na kuwawezesha kupata nafasi ya kuzikwepa**. Unabii unatangaza kwamba yule Malaika wa Kwanza alipaswa kulitoa tangazo lake kwa "kila taifa na kabila na lugha na jamaa" [Ufu. 14:6]. Onyo la Malaika yule wa Tatu [Ufu. 14:9-11], ambalo ni sehemu ya ujumbe huo wa aina tatu, halitaenea katika eneo dogo kuliko hilo. Katika unabii huo linawakilishwa kama linatangazwa **kwa sauti kuu** [Ufu. 18:1,2] na malaika yule arukaye katikati ya mbingu [Ufu. 14:6]; nalo litakuwa na uwezo wa kuyavuta mawazo ya ulimwengu mzima.

Ujumbe wa Malaika wa Tatu

"Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake." Ufunuo 14:9-11.

Makundi Mawili Yajitokeza

Katika hoja ya pambano hilo Ulimwengu wote wa Kikristo utagawanyika katika makundi makubwa mawili - wale **wazishikao amri [kumi] za Mungu** na Imani ya Yesu, na wale **wanaomsujudu mnyama na sanamu yake na kupokea chapa (alama) yake**. Ijapokuwa kanisa na serikali vitaunganisha uwezo wao ili kuwalazimisha kwa kutumia nguvu za dola "wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru na watumwa" (Ufunuo 13:16) ili wapate kupokea "chapa (alama) ya mnyama," hata hivyo, **watu wa Mungu hawataipokea**. Nabii huyo wa Patmo anawaona "wale waliokuwa wamejipatia ushindi wao dhidi ya mnyama [mfalme papa], na dhidi ya sanamu yake [Uprotestanti Asi], na dhidi ya alama yake [Jumapili], na dhidi ya hesabu ya jina lake [Vicarius Filii Dei = 666; Ufu. 13:18], walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu," nao wauimba wimbo wa Musa na wimbo wa Mwana-Kondoo [Kristo]. Ufunuo 15:2,3, KJV].

Mafundisho Makuu Mawili ya Uongo

Kwa njia ya mafundisho makuu ya uongo haya mawili, yaani, **roho isiyoweza kufa kamwe** na **utakatifu wa Jumapili**, Shetani atawaleta watu chini ya madanganyo yake. Wakati lile la kwanza linajenga msingi wa Imani ya Mizimu, lile la pili linafanya mapatano ya kushirikiana na Roma. Waprotestanti wa nchi ya Marekani watakuwa mstari wa mbele kabisa katika kuinyosha mikono yao kupitia katika ghuba na kuushika mkono wa imani ya mizimu [kutoka India na mashariki ya mbali]; watanyosha mikono yao juu ya kilindi [cha bahari] ili kushikana mikono na mamlaka ile ya Roma; na chini ya utawala wa muungano huo wa utatu [Mizimu, Uroma, na Uprotestanti Asi - Ufu. 16:13,14], nchi hii itafuata katika nyayo za Roma kwa kuzikanyaga chini ya miguu yake haki za dhamiri za watu [kuzuia watu wasimwabudu Mungu kama mioyo yao inavyotaka].

Mstari unaowatofautisha wale wanaojiita Wakristo na wale wasiomcha Mungu kwa sasa ni shida sana kuonekana. Washiriki wa kanisa wanayapenda mambo yale yale wanayoyapenda walimwengu, tena wako tayari kujiunga nao, na Shetani amedhamiria **kuwaunganisha katika shirika moja** [**la dini** - Ufu. 16:13,14; 17:1-5; 13:13,14-17,4] na kwa njia hiyo kuiimarisha kazi yake kwa kuwafagilia wote katika safu za jeshi la mizimu. Wafuasi wa papa, wanaojivunia miujiza yao kuwa ndiyo ishara ya hakika inayoonyesha kuwa kanisa lao ni la kweli watadanganywa kwa urahisi sana na mamlaka hiyo [Shetani] ifanyayo maajabu; na Waprotestanti nao, wakiwa wameitupilia

mbali ngao yao ya ile kweli [Biblia - Yn. 17:17; Zab. 119:142], pia watadanganyika. Wafuasi **wa papa, Waprotestanti wote, kwa njia ile ile moja, watakubali kuwa na mfano wa** utauwa bila kuwa na nguvu zake [bila kubadilika tabia zao], nao **wataona katika muungano wao huo tapo** [kundi] **kubwa litakalouongoa ulimwengu wote na kuikaribisha ile milenia** [miaka elfu moja] **waliyoingojea kwa muda mrefu sana**.

CHANGAMOTO TOKA ROMA

"Mhariri wa Gazeti la *Catholic Mirror* wa Baltimore, MD, alichapisha mfululizo wa makala za mhariri nne, ambazo zilitokea katika gazeti lile, Septemba 2, 9, 16 na 23, 1893…. Kwa hiyo, makala hizi, japokuwa hazikuandikwa kwa mkono wake Kadinali (Gibbons), zinatolewa chini ya kibali chake rasmi, nazo ni maelezo ya Upapa juu ya somo hili, ni changamoto ya waziwazi iliyotolewa na Upapa kwa Uprotestanti, na madai ya huo Upapa kwamba Waprotestanti watoe taarifa kwa Upapa kuonyesha kwa nini wao wanaitunza Jumapili….

"Waadventista ndilo kundi la pekee la Wakristo ambalo linaitegemea Biblia kama mwalimu wao, ambao katika kurasa zake hawaoni amri yo yote inayoruhusu badiliko la siku kutoka ile ya saba kwenda ile ya kwanza. Hivyo wanaitwa jina lao 'Waadventista wa Siku ya Saba (Seventh-day Adventists).'… Waprotestanti … wameikataa katakata siku ya ibada iliyotajwa kwa jina lake [Sabato], na kwa kinyume dhahiri na amri yake, kutwaa siku ya ibada ya kumwabudu yeye ambayo haikupata kutajwa kamwe kwa kusudi hilo katika kurasa za Gombo hilo Takatifu [Biblia]….

"Lakini ukweli, jambo la hakika, na la haki, yaani, maana ile halisi ya haki inatukataza sisi kulishutumu dhehebu hilo dogo sana [Waadventista Wasabato ambao leo idadi yao ni zaidi ya milioni tisa] bila kuwa na uchunguzi uliofanywa kwa utulivu na bila kupendelea upande wo wote….

"Ulimwengu wa Kiprotestanti, tangu kuzaliwa kwake katika karne ile ya kumi na sita, umeafikiana kabisa na Kanisa Katoliki katika "kuitakasa" sio Jumamosi, bali Jumapili.

"Endapo … kwa upande mwingine hao wa mwisho watatoa sababu zisizoweza kukanushwa na umati mkubwa wa Waprotestanti… [Waprotestanti] … hawana njia yo yote nyingine ya kufuata kuliko ile ya kukubali kuwa wamekuwa wakifundisha na kuifuata desturi potofu kimaandiko kwa zaidi ya karne tatu [kufikia 1893]…. Kuongezea juu ya kosa hilo zito [kubwa] la Kimaandiko, lisilosameheka, suala hilo linahusu mojawapo ya amri hai, yenye nguvu ya Mungu kwa mtumishi wake, kwa mwanadamu, isemayo: "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase." (Hiyo ni siku ya saba [Jumamosi]). Hakuna Mprotestanti hata mmoja aliye hai leo (ukiwaacha Waadventista na wengine wachache) aliyepata kuitii amri hiyo, wakipendelea kulifuata kanisa lililoasi wanalolitaja-taja hivyo kuliko kumfuata mwalimu wao, yaani, Biblia, ambayo, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, haifundishi fundisho jingine lo lote…." *Rome's Challenge*, 1-5.

"Kwa hiyo hitimisho lake haliepukiki; yaani, la wale wanaoifuata Biblia kama kiongozi wao, Waisraeli na Waadventista Wasabato wanao uzito wa pekee wa ushahidi kwa upande wao, ambapo Mprotestanti wa Biblia hana neno hata moja la kujitetea kwa kuiweka Jumapili mahali pa Jumamosi." k.k.k. [kitabu kile kile], uk. 11.

Shetani, Mpanzi ya Uovu, Alitoka Wapi?

Chimbuko la Dhambi

Katika mawazo ya watu wengi chimbuko la uovu na sababu ya kuwapo kwake ni chanzo cha utata mkubwa sana kwao. Wanaona matendo mabaya, pamoja na matokeo yake ya kutisha yaletayo misiba na maangamizi, nao huuliza kwamba mambo hayo yote yanawezaje kuwapo chini ya utawala wa yule Mmoja aliye na hekima, uweza, na upendo usio na kikomo.

Ni jambo lisilowezekana kabisa kueleza chimbuko hilo la dhambi kwa kiasi cha kuweza kutoa sababu ya kuwapo kwake. Lakini kinaweza kufahamika kiasi cha kutosheleza kwa mambo haya mawili, chimbuko la dhambi na kuondolewa kwake hatimaye, ili kudhihirisha kwa ukamilifu haki na fadhili zake Mungu katika kuushughulikia kwake kote uovu huo. Dhambi ni kitu kinachojiingiza chenyewe, kuwako kwake hakuna sababu iwezayo kutolewa. Kama udhuru wo wote ungeweza kupatikana wa kuwako kwa dhambi hiyo, au sababu yo yote ingeweza kutolewa kwa kuwako kwake, basi, ingekoma kuwa dhambi. Maana ya dhambi tuliyo nayo peke yake ni ile iliyotolewa katika Neno la Mungu; yaani, [**dhambi**] **ni uvunjaji wa Sheria** [Amri Kumi - 1 Yohana 3:4, AJKK]."

Upendo wa Mungu dhidi ya Kiburi

Sheria ile ya upendo [Amri Kumi - Mt. 22:35-40; Rum. 13:8-10; Yak. 2:10-12] ikiwa ndiyo **msingi wa Serikali ya Mungu**, basi, kule kuafikiana kabisa na kanuni zake za haki lilikuwa ndilo tegemeo la furaha ya viumbe vyote vilivyoumbwa. Mungu anataka huduma ya upendo toka kwa viumbe vyake vyote - yaani, ibada ile itokanayo na kuithamini tabia yake kwa kutumia akili zetu. Haufurahii utii unaotolewa kwake kwa kujilazimisha, tena yeye huwapa wote uhuru wa kufanya wapendavyo, ili waweze kumpa huduma yao ya hiari. Lakini alikuwako mmoja aliyechagua kuutumia vibaya uhuru wake. **Dhambi ilianzishwa na huyo**, ambaye, akiwa wa pili toka kwa Kristo, alikuwa amepewa heshima kubwa sana, naye alikuwa amesimama mahali pa juu sana pa mamlaka na utukufu miongoni mwa wakazi wote wa mbinguni. Kabla ya anguko lake, Lusifa [Lucifer = Nyota ya Alfajiri - Isa. 14:12, KJV] alikuwa Kerubi afunikaye wa kwanza, mtakatifu, na asiye na waa. Angalia Ezekieli 28:12-15.

Lusifa angeweza kubakia katika upendeleo wa Mungu, akiwa anapendwa na kuheshimiwa na jeshi lote la malaika, akitumia uwezo wake mkuu kuwaletea furaha wengine na kumtukuza Muumbaji wake. Lakini, asema hivi huyo nabii, "Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako." Ezekieli 28:17. Kidogo kidogo, Lusifa akaanza kuingiwa na tamaa ya kujikweza mwenyewe. "Nawe ulisema … Nitapaa kupita vimo vya mawingu, **Nitafanana na Yeye Aliye Juu**." Isaya 14:13,14. Badala ya yeye kumfanya Mungu aonekane kuwa ndiye Mkuu

kuliko wote katika mapenzi na utiifu wa viumbe vyake, ilikuwa ni jitihada yake Lusifa kuwashawishi watoe huduma yao pamoja na utii wao kwake yeye mwenyewe. Naye akiwa anatamani sana heshima ile ambayo Baba wa milele alikuwa amempa Mwanawe, mkuu huyo wa malaika akataka sana kujinyakulia mamlaka yale ambayo ilikuwa ni haki yake Kristo peke yake kuyatumia.

Mwana wa Mungu alikuwa ndiye Mfalme wa mbinguni aliyetambulikana hivyo, akiwa na uweza na mamlaka kama Baba yake. Katika mashauri ya Mungu, Kristo alishiriki, ambapo Lusifa hakuruhusiwa hivyo kuingia katika makusudi ya Mungu. "Kwa nini Kristo awe mkuu kuliko wote"? akauliza yule malaika mwenye uwezo mwingi, "Kwa nini yeye anaheshimiwa kuliko mimi Lusifa?"

Ajivika Usiri

Shetani alikuwa amepewa heshima kubwa sana, na matendo yake yote yalikuwa na usiri, hata ikawa vigumu [kwa Mungu] kuwafunulia malaika wale hali halisi ya kazi yake. Mpaka hapo itakapofikia ukamilifu wake, dhambi isingalionekana kuwa ni kitu kibaya kama vile ilivyo. Mpaka wakati ule ilikuwa haina nafasi yo yote katika malimwengu ya Mungu, wala viumbe wale watakatifu hawakuwa na wazo lo lote kuhusu hali yake halisi, wala ubaya wake. Hawakuweza kutambua athari zake zitakazotokea kwa kitendo cha kuiweka kando Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Katika kuishughulikia dhambi, Mungu angeweza kutumia haki na kweli tupu. Shetani angeweza kutumia kile ambacho Mungu asingeweza kutumia - yaani, kujipendekeza na udanganyifu. Hali ile ya kutokuelewana iliyosababishwa na mwenendo wake kule mbinguni, Shetani akailaumu Sheria [Amri Kumi] na Serikali ya Mungu [kuwa ndicho chanzo chake]. Akatangaza kwamba maovu yote yalikuwa ni matokeo ya utawala wa Mungu. Akadai kwamba lilikuwa ni lengo lake kuziboresha Sheria za Yehova. Kwa ajili hiyo, ilikuwa ni lazima kwamba aonyeshe sura ya madai yake, na kuonyesha utendaji wa mabadiliko yake aliyokuwa amependekeza yafanyike katika Sheria ile ya Mungu [Amri Kumi]. Kazi yake ni lazima imhukumu mwenyewe. Tangu mwanzo Shetani alikuwa amedai kwamba alikuwa hajafanya maasi yo yote. Ni lazima apewe muda wa kujifunua mwenyewe kwa kazi zake za uovu. Ulimwengu wote unapaswa kumwona laghai huyo akiwa amefuchuliwa.

Roho Ile Ile

Roho ile ile iliyochochea maasi kule mbinguni bado inaendelea kuchochea maasi hapa duniani. Shetani ameendelea kushughulika na wanadamu kwa kutumia mbinu yake ile ile aliyoitumia kwa wale malaika. Kwa njia ile ile ya kuieleza vibaya tabia ya Mungu kama vile alivyofanya mbinguni, alipomfanya [Mungu] afikiriwe kuwa ni mkali tena ni dhalimu, Shetani alimshawishi mwanadamu kutenda dhambi. Na baada ya kufanikiwa mpaka pale, akatangaza kwamba vizuio vyote vya Mungu ambavyo vilikuwa si vya haki ndivyo vilivyosababisha mwanadamu kuanguka dhambini, kama vile vilivyomfanya yeye kuangukia katika maasi yale. Mungu alitoa ushahidi wa upendo wake kwa kumtoa Mwanawe pekee kufa kwa ajili ya wanadamu walioanguka [dhambini - Yn. 3:16]. Katika upatanisho huo tabia ya Mungu imedhihirika. Hoja ile yenye nguvu ya msalaba hudhihirisha kwa malimwengu yote kwamba, kwa vyo vyote vile, Serikali ya Mungu isingestahili kutupiwa lawama yo yote kutokana na njia ile ya dhambi aliyoichagua Lusifa.

Ni Zaidi ya Ukombozi

Haikuwa kwa ajili ya kujipatia ukombozi wa mwanadamu tu ya kwamba Kristo alikuja humu duniani kuteswa na kufa. Alikuja "**kuitukuza Sheria [Amri Kumi]** na "**kuiadhimisha**" [Isa. 42:21; Mt. 5:17-48]. Sio tu kwamba wakazi wa ulimwengu huu wapate kuitunza Sheria yake [Amri Kumi] kama inavyopasa kutunzwa, bali ilikuwa ni kwa madhumuni ya kuzionyesha dunia zote za malimwengu kwamba **Sheria ya Mungu [Amri Kumi] haibadiliki**. Endapo madai yake yangeweza kuwekwa kando, basi, Mwana wa Mungu naye **asingelazimika kuutoa uhai wake ili kufanya upatanisho kwa ajili ya uvunjaji wa Sheria hiyo [Amri Kumi]**. **Kifo cha Yesu kinathibitisha kwamba Sheria hiyo [Amri Kumi - Kut. 20:3-17] haibadiliki kamwe**.

Katika utekelezaji ule wa mwisho wa hukumu itadhihirika ya kwamba **hapakuwa na sababu yo yote ya kuwako dhambi**. Msalaba ule wa Kalvari, wakati unatangaza kwamba Sheria [Amri Kumi] haibadiliki, wakati uo huo unatangaza kwa malimwengu yote kwamba **mshahara wa dhambi [kuvunja Amri Kumi] ni mauti**. Katika kile kilio cha mwisho alicholia Mwokozi, akisema, "**Imekwisha**," **kengele ya kifo cha Shetani iligongwa**. Pambano kuu lililokuwa limeendelea sana likaamuliwa wakati ule, na hatua ya mwisho ya kuzifutilia mbali dhambi ikathibitishwa. Malimwengu yote yatakuwa yameshuhudia tabia na matokeo ya dhambi.

Shetani Auongoza Mpango wa Ulimwengu Mpya

Kwa njia ya Imani ya Mizimu, Shetani anaonekana kwao kama ni mfadhili wa wanadamu, anayeponya magonjwa ya watu, tena yeye anadai kwamba **analeta mfumo mpya na ulio bora zaidi wa imani ya dini**; lakini wakati uo huo anafanya kazi yake kama **mwangamizaji wa watu**. Majaribu yake yanawapeleka watu wengi kwenye maangamizi. Ulevi huiondoa busara toka kwenye kiti chake cha enzi [ubongoni]; hapo ndipo hufuata mambo ya kujifurahisha katika tamaa zao mbaya za mwili, magomvi, na umwagaji wa damu. Shetani anafurahia sana vita, kwa maana inachochea harara mbaya mno za moyoni na kuwafagia kuingia katika umilele wao wahanga wake wakiwa wamezama katika dhambi zao na damu. Ni lengo lake **kuyachochea mataifa kupigana vita yenyewe kwa yenyewe**, maana kwa njia hiyo anaweza kuigeuza mioyo ya watu kuacha kazi ya kujiweka tayari kwa siku ile ya Mungu. Shetani pia anafanya kazi yake kupitia katika matetemeko ya nchi, mafuriko, uchafuzi wa angahewa na mazingira pamoja na moto ili kuvuna mavuno yake ya watu wasiokuwa tayari [wasiojitoa kikamilifu kwa Yesu]. Amefanya utafiti na kujifunza siri za viumbe vile vya asili [maumbile] katika maabara zake, naye hutumia uwezo wake wote kudhibiti ardhi, maji, hewa, na moto kwa kadiri Mungu anavyomruhusu. Aliporuhusiwa kumtesa Ayubu, kwa haraka jinsi gani aliweza kufagilia mbali makundi yake ya kondoo na ng'ombe, watumishi wake, nyumba yake, watoto wake, taabu moja ikafuata baada ya nyingine kwa muda mfupi sana. Ni Mungu anayevilinda viumbe vyake na

kuvizungushia ugo ili kuvilinda mbali na uwezo wa huyo mwangamizaji. Lakini Ulimwengu huu wa Kikristo umeonyesha dharau kubwa sana dhidi ya Sheria yake Yehova [Amri Kumi]; na Bwana atafanya kile alichotangaza kuwa atafanya - ataiondoa mibaraka yake toka duniani na kuondoa ulinzi wake kwa wale wanaoendelea kufanya maasi dhidi ya Sheria yake [Amri Kumi], **wanaowafundisha na kuwalazimisha wengine kufanya vivyo hivyo** [Mt. 5:17-19]. **Shetani anawadhibiti kabisa wale wote ambao Mungu hawalindi**. [Shetani] atawapendelea na kuwafanikisha wengine ili kuendeleza mipango yake mwenyewe, na wengine atawaletea taabu na kuwafanya watu wasadiki kwamba ni Mungu anayewatesa.

Wakati ule ule yeye [Shetani] anapojitokeza kwa wana wa wanadamu kama tabibu mkuu awezaye kuyaponya maradhi yao yote, **atawaletea magonjwa na maafa mpaka miji iliyojaa watu wengi sana itakapokuwa imebaki magofu na ukiwa** [Isa. 6:8-11].

Wataabishaji wa Watu Watambulishwa

Na wakati ule ndipo laghai huyo atakapowashawishi wanadamu, na kuwaambia kwamba wale wanaomtumikia Mungu ndio wanaosababisha maovu hayo. Kundi lile lililoichokoza ghadhabu ya Mbingu ndilo litakalowashutumu wale ambao utii wao kwa zile amri [kumi] za Mungu ni kemeo la kudumu kwa wale wanaozivunja Amri Kumi, litasema kwamba hao ndio waliowaletea taabu zao zote. Itatangazwa kwamba watu hao wanamchukiza Mungu kwa kuivunja sabato yao ya Jumapili; ya kwamba dhambi hiyo imeleta misiba ambayo haitakoma mpaka utunzaji wa Jumapili utakapolazimishwa kwa ukali sana kwa kuutungia sheria Bungeni; na ya kwamba wale wanaotoa madai ya kuitunza ile amri ya nne [Kut. 20:8-11], kwa njia hiyo wanaharibu heshima kuu inayotolewa kwa Jumapili, hao ndio wataabishaji wa watu, hao ndio wanaowazuia wao wasipate kurejeshwa katika upendeleo wa Mungu na usitawi wa dunia hii. Nguvu hiyo itendayo miujiza [Shetani] ambayo inajidhihirisha kupitia katika ile Imani ya Mizimu itaushinikiza uwezo wake dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Ujumbe kutoka kwa hayo mapepo utatangaza kwamba Mungu amewatuma kuja kuwahakikishia kosa lao wale wanaoikataa Jumapili, watathibitisha kwamba sheria za nchi [serikali] zingepaswa kutiiwa kama Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Wataomboleza kwa ajili ya uovu mkuu uliomo duniani na kuunga mkono ushuhuda wa waalimu wale wa dini usemao kwamba mmomonyoko huo wa maadili umesababishwa na kuinajisi Jumapili. Hasira itakuwa ni kali mno ambayo itachochewa dhidi ya wale wote wanaokataa kuukubali ushuhuda wao.

"Iliuchukua Upapa ule na taasisi zake zilizowekwa, yaani, Kanisa Katoliki la Roma, takriban miaka 2000 kufikia hadhi na nafasi yake katika jamii na kuwa dini ya ulimwengu mzima…. Je, ulikuwa na mkakati wake wa kisiasa na muundo wake? Naam, ulikuwa na mkakati wake wa kisiasa na muundo wa ulimwengu mzima. Kwa maana, mwisho wake, Yohane Paulo II kama mdai aliye Badala ya Kristo (Vicar of Christ [au Vicarius Filii Dei]) anadai kwamba yeye ndiye mahakama ya mwisho ya hukumu juu ya jamii ya mataifa yote yakiwa kama jamii moja." *Keys of This Blood*, **M. Martin, ukurasa 374-375.**

Shetani Aja Katika Umbile la Kristo

Kama tendo lake la kilele katika mfululizo wa matukio makuu ya udanganyifu wake, Shetani atakuja mwenyewe akiwa na umbile linalofanana kabisa na lile la Kristo. Kanisa limetangaza kwa muda mrefu sana kwamba linatazamia kumwona Mwokozi akija mara ya pili kuja kutimiza matumaini yake. Basi huyo laghai mkuu [Shetani] atafanya ionekane kana kwamba Kristo amekuja. Katika sehemu mbalimbali za dunia, Shetani atajionyesha mwenyewe miongoni mwa wanadamu kama kiumbe mwenye utukufu, anayeng'aa kwa mng'ao unaotia macho kiwi, akifanana na maelezo ya umbile la Mwana wa Mungu [Kristo] yaliyotolewa na Yohana katika Ufunuo 1:13-15. Utukufu ule unaomzunguka pande zote haufanani na kitu cho chote ambacho macho ya wanadamu yamepata kukiona. Makelele ya shangwe yanavuma hewani: "Kristo amekuja! Kristo amekuja!" Watu wanaanguka kifudifudi mbele yake na kumsujudu, wakati yeye anainua mikono yake juu na kutamka baraka juu yao, kama vile Kristo alivyowabariki wanafunzi wake alipokuwa hapa duniani. Sauti yake ni nyororo na tulivu, lakini ni tamu sana kama muziki. Kwa sauti ya upole, yenye huruma, anazihubiri baadhi ya kweli zile zile za thamani za mbinguni, ambazo Mwokozi alizinena; anaponya magonjwa ya watu, halafu katika tabia yake ya kuigiza ya Kristo, anadai kwamba ameibadili Sabato [Jumamosi] kuwa Jumapili, naye anawaamuru wote kuitakasa siku hiyo [ya Jumapili] aliyoibariki yeye. Anatangaza kwamba wale wanaoendelea kuitakasa siku ile ya saba [Jumamosi] wanalikufuru jina lake kwa kukataa

kuwasikiliza malaika zake aliowatuma kuleta nuru na kweli. Hayo ndiyo madanganyo yake yenye nguvu nyingi sana yanayowashinda nguvu karibu watu wote. Kama vile Wasamaria wale walivyodanganywa na Simoni Mchawi (Magus), ndivyo watu wengi sana, kuanzia aliye mdogo sana mpaka aliye mkubwa kuliko wote, wanasikiliza uchawi huo, na kusema: Huu ni "uweza ule mkuu wa Mungu." Matendo 8:10, KJV.

Kumng'amua Laghai Huyo

Lakini **watu wa Mungu hawatapotoshwa**. Mafundisho ya kristo huyo wa uongo hayapatani na Maandiko. Baraka yake inatamkwa juu ya wale wanaomsujudu yule mnyama na sanamu yake, yaani, kundi lile lile hasa ambalo juu yake Biblia inatangaza kwamba ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na maji itamwagwa.

Tena, zaidi ya hayo, **Shetani haruhusiwi kuigiza namna Kristo atakavyokuja mara ya pili**. Mwokozi amewaonya watu wake dhidi ya udanganyifu katika suala hilo, tena ametabiri waziwazi jinsi kuja kwake mara ya pili kutakavyokuwa. "Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa [miujiza mikubwa] na maajabu; **wapate kuwapoteza**, yamkini, hata walio wateule…. Basi, wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; Yumo nyumbani [yumo katika vyumba vya siri - KJV], msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Mathayo 24:24-27; 25:31; Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16,17(18). Kuja huko hakuna uwezekano wo wote wa kukuigiza. Kutajulikana ulimwenguni kote - kutashuhudiwa na ulimwengu wote.

Ni Biblia Peke Yake

Ni wale tu waliokuwa wanafunzi wa Maandiko wenye bidii, walioupokea upendo wa ile kweli [walioiweka kweli katika matendo yao] ambao watalindwa kutokana na madanganyo yale yenye nguvu sana yatakayouteka ulimwengu wote. Kwa ushuhuda wa Biblia watamng'amua mdanganyaji huyo anayejigeuza umbile lake ili kudanganya. Wakati ule wa kujaribiwa utawajia watu wote [Ufu. 3:10]. Kwa njia ya kupepetwa na majaribu ndipo Mkristo wa kweli atakapoonekana. Je, hivi watu wa Mungu siku hizi wamejizatiti kabisa juu ya neno lake kiasi kwamba hawawezi kusalimu amri kwa hisia zao? Je, katika wakati wa hatari kama huo wangeweza kuing'ang'ania Biblia na Biblia peke yake? Shetani, ikiwezekana, atawazuia wasiweze kujitayarisha kusimama katika siku ile. Atayapanga mambo kwa njia ambayo itaifanya njia yao izungushiwe boma, atawanasa kwa kuwafanya wabebe mzigo mzito ulemeao, hata mioyo yao italemewa na masumbufu ya maisha haya na siku ile ya kujaribiwa itaweza kuwajia kama mwivi.

La Kufanya Sasa ni Lipi

Imani na Kupokea

Dhamiri yako imekwisha kuchomwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu fulani juu ya ubaya wa dhambi, hatia yake, matatizo yake; nawe unaiangalia kwa chuki kubwa. Unahisi kwamba dhambi hiyo imekutenga mbali na Mungu, kwamba wewe umekuwa mtumwa kwa kuzidiwa nguvu na uovu huo. Kadiri unavyojitahidi kuukwepa, ndivyo kadiri unavyotambua kwamba huna uwezo wo wote wa kupigana nao. Makusudi yako ni machafu; moyo wako si safi. Unaona kwamba maisha yako yamejaa uchoyo na dhambi. Unatamani kusamehewa, kutakaswa, kuwa huru. Kuwa na amani na Mungu wako, kufanana naye - je, hivi ufanye nini ili uwe na hali hiyo?

Ni amani unayoihitaji, - yaani, msamaha toka Mbinguni na amani na upendo moyoni mwako. Fedha haiwezi kuinunua, akili nyingi haziwezi kuipata, hekima haiwezi kuifikia; kamwe huwezi kutumaini kuipata kwa juhudi zako mwenyewe. Lakini Mungu anakupa wewe kama zawadi, "bila fedha na bila thamani" (Isaya 55:1). Ni yako kama wewe utanyosha mkono wako na kuishika sana. Bwana asema hivi, "Dhambi [za]ko zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu" (Isaya 1:18). "Nami nita[ku]pa [wewe] moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani ya mwili [wako]" (Ezekieli 36:26).

Umekwisha kuziungama dhambi zako, na moyoni mwako umezitupilia mbali. Umeazimu kujitoa mwenyewe kwa Mungu. Basi nenda kwake, na kumwomba azioshe dhambi zako na kuziondoa mbali nawe, na kukupa wewe moyo mpya. Kisha

amini kwamba anakufanyia hivyo *kwa kuwa yeye ndiye aliyeitoa ahadi hiyo kwako*. Hili ndilo fundisho alilolifundisha Yesu alipokuwa hapa duniani, ya kwamba zawadi anayotuahidi Mungu, ni lazima sisi tuamini kwamba tumekwisha kuipokea, nayo inakuwa yetu. Yesu aliwaponya watu magonjwa yao walipouamini uwezo wake; aliwasaidia katika mambo yale waliyoweza kuyaona, hivyo kuwatia imani kwake kwa mambo yale ambayo hawakuweza kuyaona kwa macho yao, - akiwaongoza wapate kuuamini uwezo wake wa kusamehe dhambi. Jambo hilo alilisema waziwazi alipomponya mtu yule aliyekuwa na ugonjwa wa kupooza: "*Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anao uwezo duniani wa kusamehe dhambi*, (amwambia yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako" (Mathayo 9:6, KJV). Vivyo hivyo Yohana, yule Mwinjilisti, asema hivi pia, akiongea juu ya miujiza yake Kristo, "Lakini hizi [ishara = miujiza] zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu, na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake" (Yohana 20:31).

Kutokana na maelezo rahisi ya Biblia kuhusu jinsi Yesu alivyowaponya wagonjwa, sisi tunaweza kujifunza kitu fulani juu ya namna ambavyo sisi tunaweza kumwamini kwa ajili ya msamaha wa dhambi zetu. Hebu na tuangalie kisa cha mtu yule aliyepooza pale Bethzatha. Maskini yule aliyeteseka alikuwa hana uwezo wo wote; alikuwa hajavitumia viungo vyake vya mwili kwa miaka thelathini na minane. Licha ya kuwa na hali hiyo, Yesu akamwamuru, akasema, "Simama, jitwike godoro lako, uende" [Yohana 5:8,9]. Mtu yule mgonjwa angeweza kusema, "Bwana, ukinifanya mzima, ndipo mimi nitalitii neno lako." Lakini, la, aliliamini neno lake Kristo, aliamini kwamba *alikuwa amefanywa mzima*, ndipo akafanya jitihada yake mara

moja; *akanuia* kutembea, naye kweli alitembea. Alitenda kwa kulifuata neno lake Kristo, na Mungu akampa uwezo ule. Akawa mzima.

Vivyo hivyo wewe nawe u mwenye dhambi. Huwezi kulipa fidia kwa ajili ya dhambi zako zilizopita, huwezi kuubadilisha moyo wako, na kujifanya mtakatifu wewe mwenyewe. Lakini Mungu anakuahidi kukufanyia wewe yote hayo kwa njia ya Kristo [1 Yohana 1:9]. Wewe *unaiamini* ahadi ile. Unaziungama dhambi zako, na kujitoa mwenyewe kwa Mungu. *Unanuia* kumtumikia. Kwa hakika kama unavyofanya hivyo, Mungu atalitimiza neno lake kwako. Ukiiamini ahadi hiyo, - yaani, ukiamini kwamba umesamehewa na kutakaswa, - Mungu anakutendea tendo hilo; unakuwa mzima, sawasawa kabisa na jinsi Kristo alivyompa mtu yule aliyepooza nguvu kuweza kutembea wakati mtu yule alipoamini kwamba ameponywa. Inakuwa *hivyo* ukiamini.

Usingoje *kujisikia moyoni mwako* kama umekuwa mzima [kweli], bali sema, "Naamini; mambo *ni hivyo*, si kwa sababu mimi najisikia ndani yangu, bali *kwa sababu Mungu ameniahidi hivyo*."

Yesu asema hivi, "Yo yote myaombayo mkisali, *aminini kwamba mnayapokea*, nayo yatakuwa yenu" (Marko 11:24). Kuna sharti moja linaloambatana na ahadi hiyo, - kwamba sisi tuombe kulingana na mapenzi ya Mungu. Lakini basi, ni mapenzi ya Mungu kutusafisha dhambi zetu, kutufanya watoto wake, na kutuwezesha sisi kuishi maisha matakatifu. Kwa hiyo tunaweza kuomba atupe sisi mibaraka hiyo, na *kuamini kwamba tunaipokea*, na *kumshukuru Mungu* kwamba sisi *tumekwisha* kuipokea. Ni fursa yetu kwenda kwa Yesu na kutakaswa, halafu kusimama mbele ya Sheria [Amri Kumi - Yak. 1:25] bila kuona

haya, wala majuto. "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, *wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho*" (Warumi 8:1, KJV).

Kuanzia sasa na kuendelea wewe si mali yako mwenyewe; umenunuliwa kwa thamani [1 Kor. 6:19,20]. "Mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, fedha au dhahabu,… bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo" (1 Petro 1:18,19). Kupitia katika tendo hilo rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amekwisha kukupa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni kama mtoto mchanga aliyezaliwa katika familia ya Mungu, naye anakupenda wewe kama anavyompenda Mwanawe.

Sasa, basi, kwa kuwa wewe umejitoa mwenyewe kwa Yesu, usirudi nyuma, yaani, usijiondoe kwake, lakini siku kwa siku sema, "Mimi ni wake Kristo; nimejitoa kwake;" nawe mwombe yeye akupe Roho Mtakatifu, na kukulinda kwa neema yake [Rum. 8:8-11,14; 2 Kor. 12:9,10; Yuda 24]. Kama ilivyo ya kwamba wewe ukijitoa mwenyewe kwa Mungu, na kumwamini, unakuwa mtoto wake [Yn. 1:12,13], hivyo ndivyo ikupasavyo kuendelea kuishi ndani yake. Mtume huyu asema hivi: "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, *enendeni vivyo hivyo* katika yeye" (Wakolosai 2:6).

Wengine moyoni mwao wanajisikia kana kwamba ni lazima wajipime wenyewe kwa kufanya mambo fulani mema, na kuona kwamba ni lazima wamhakikishie Bwana ya kwamba wao wamebadilika kabisa, kabla hawajaweza kuudai mbaraka wake. Lakini basi, wao wanaweza kuudai mbaraka huo wa Mungu hata sasa. Ni lazima wapate neema yake, Roho wake Kristo, kuwasaidia katika udhaifu wao, vinginevyo hawawezi kuupinga uovu. Yesu anapenda kutuona sisi tukija kwake jinsi

tulivyo, yaani, tukiwa wenye dhambi, tusio na uwezo wo wote, tunaomtegemea yeye. Twaweza kuja kwake pamoja na udhaifu wetu wote, upumbavu wetu wote, na hali yetu ya kutenda dhambi, halafu kuanguka miguuni pake kwa toba. Kwake ni utukufu kutukumbatia sisi kwa mikono yake ya upendo, na kutufunga majeraha yetu, na kutusafisha uchafu wetu wote.

Hapo ndipo ambapo maelfu hushindwa: hawaamini kwamba Yesu anawasamehe wao binafsi, yaani, kila mmoja peke yake. Hawamwamini Mungu asemavyo katika neno lake. Ni fursa ya wote wanaotimiza masharti hayo kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa bure kwao kwa kila dhambi waliyotenda. Basi, tupilia mbali mashaka yako yanayokuambia kwamba ahadi za Mungu hazikutolewa kwa ajili yako wewe. Ahadi hizo ni kwa kila mvunja Sheria [Amri Kumi] atubuye. Nguvu na neema imetolewa kwa njia ya Kristo na kuletwa na malaika wale wanaohudumu kwa kila mtu aaminiye. Hakuna walio wabaya kupindukia kiasi cha kutoweza kupata nguvu, usafi wa maisha, na haki ndani ya Yesu, aliyewafia. Yeye anangojea ili apate kuwavua mavazi yao yaliyotiwa mawaa na kuchafuliwa na dhambi, na kuwavika mavazi meupe ya haki [Zek. 3:1-5; Isa. 61:10]; anawaamuru waishi, wala wasife.

Mungu hatushughulikii sisi kama wanadamu wanavyoshughulikiana wenyewe kwa wenyewe. Mawazo yake ni mawazo yaliyojaa huruma, upendo, na upole unaosikitika pamoja nasi tunapoteseka [Isa. 63:9; Ebr. 2:17; 4:14-16]. Yesu asema, "Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye *atamsamehe kabisa*" (Isaya 55:7). "Nimeyafuta makosa yako kama wingu zito, na dhambi zako kama wingu" (Isaya 44:22).

"Maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini [rudini], mkaishi" (Ezekieli 18:32). Shetani yuko tayari kukupora wewe zile ahadi za Mungu zenye mibaraka. Anatamani kuiondoa kila nuru iliyo ndogo ya tumaini ulilo nalo na kila mwonzi wa nuru kutoka moyoni mwako; lakini wewe ni lazima usimruhusu akufanyie hivyo. Usitege sikio lako kumsikiliza mjaribu huyo, bali umwambie hivi: "Yesu alikufa ili mimi nipate kuishi. Ananipenda, wala hataki mimi niangamie. Ninaye Baba yangu mwenye huruma kule mbinguni; na japo mimi nimeuchezea vibaya sana upendo wake, japo mibaraka aliyonipa nimeitapanya ovyo, nitaondoka, nitakwenda kwa Baba yangu, na kumwambia, 'Nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako'" Mfano huo unakuambia wewe jinsi mwana mpotevu atakavyopokewa: "*Alipokuwa angali mbali*, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana" (Luka 15:18-20).

Wewe ukiwa na ahadi hizo nyingi za Biblia mbele yako, je, unaweza kuyapa nafasi mashaka yako? Je, unaweza kuamini kwamba mwenye dhambi maskini anapotamani sana kurudi, yaani, anapotamani sana kuziacha dhambi zake, Bwana humzuia kwa ukali asiweze kuja miguuni pake kwa toba? Achana kabisa na mawazo kama hayo! Hakuna cho chote kiwezacho kukuumiza moyo wako sana kuliko kuikaribisha dhana kama hiyo juu ya Baba yetu aliye mbinguni. Yeye anaichukia dhambi, bali anampenda mwenye dhambi, naye alijitoa nafsi yake kwa njia ya Kristo, ili wale watakao wapate kuokolewa, na kupata furaha ya milele katika ufalme ule wa utukufu. Ni lugha gani yenye nguvu au upole ambayo ingeweza kuwa imetumika kuliko ile aliyoichagua yeye kuelezea upendo wake alio nao kwetu sisi?

Anatangaza, anasema, "Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe." Isaya 49:15.

Tazama juu, wewe unayeona mashaka moyoni mwako na kutetemeka; kwa maana Yesu yu hai kutuombea sisi. Mshukuru Mungu kwa zawadi ya Mwanawe mpendwa aliyokupa wewe, kisha omba kwamba asingeweza kufa bure kwa ajili yako. Roho anakualika leo. Njoo kwa moyo wako wote kwa Yesu, nawe unaweza kuudai mbaraka wake.

Unapozisoma ahadi zake, kumbuka kwamba hizo zinaonyesha upendo wake usioneneka pamoja na huruma yake kwako. Moyo ule mkuu wa Upendo wa Mungu unavutwa kuelekea kwa mwenye dhambi ukiwa na huruma isiyo na mipaka. "Kwa damu yake tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi." Waefeso 1:7. Naam, amini tu kwamba Mungu ndiye msaada wako. Anataka kuirejesha sura yake ya kimaadili ndani ya mwanadamu. Unapokwenda karibu naye kwa ungamo na toba, yeye naye atakuja karibu nawe akiwa na rehema na msamaha wake.

Yesu Mwokozi, kwa hakika, Hunipa furaha na amani; Mrithi wa wokovu wake, Natakaswa kwa damu yake. Habari hiyo wimbo wangu, Daima nitamsifu Yesu. Habari hiyo wimbo wangu, Daima nitamsifu Yesu. Nijitoapo nina raha, Na kwa imani namwona Bwana; Aniletea malaika, Wananilinda, niokoke. Hali na mali anaitwaa, Katika Yesu nabarikiwa; Nikimngoja kwa subira, Wema wake unanitosha. (E.G.White, *Steps to Christ*, Chapter 6, Faith and Acceptance)

ONYO LA MWISHO KWA DUNIA

MPANGO WA ULIMWENGU MPYA

Ni Mataifa Makuu ya Ulimwengu Mangapi Yamesalia?

"AMANI duniani" ni wazo kuu linaloenezwa kwa watu mara moja kila mwaka na Ulimwengu wa Kikristo wanaposherehekea Sikukuu ya Kuzaliwa Yesu. Kwa kweli, watu wema kila mahali hawatamani kitu kingine cho chote zaidi ya kuwa na amani hapa duniani ili wapate kuuonja utamu wa furaha katika familia yao, imani yao moja, pamoja na marafiki zao, na kuonja matunda ya kazi yao ngumu iliyofanywa kwa uaminifu. Lakini ni jinsi gani amani hiyo ya dunia inavyoonekana kuteleza!

Dunia hii imepitia katika vipindi mbalimbali vya amani ya kisiasa na kijamii wakati wa zile dola kuu za ulimwengu kama vile Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani, na Roma. Historia imeandika vizuri kumbukumbu zinazoonyesha kwamba wakati ule wa kuanguka kwa dola ya Roma, Ulaya ilisambaratika na kuwa mataifa mbalimbali kumi. Kupitia katika karne hizo nyingi, maelfu na hata mamilioni ya watu wameangamizwa wakati watu mbalimbali wenye nguvu walipojaribu bila mafanikio kuzirudisha sehemu hizo zilizosambaratika ili ziwe pamoja tena.

Vita Kuu ya Kwanza ilipiganwa kwa madhumuni yale yaliyokusudiwa ya "kukomesha vita." Kutokuwa na maana kwa dai lile kulionekana waziwazi katika moto ule mkubwa uliolipuka wakati wa Vita Kuu ya Pili. Vita hiyo ya ulimwengu mzima ilifikia tu mwisho wake hasa hasa wakati ule ulipotokea uvumbuzi na matumizi ya nguvu ya nyuklia inayozishangaza

mno akili zetu. Wakati wa macheo ya kipindi cha mabomu ya atomu wanadamu waliunda silaha za maangamizi zenye nguvu nyingi mno na za kuogofya mno kiasi kwamba tumeingiwa na hofu kwamba pambano lo lote linaweza kutuelekeza kwenye maangamizi makubwa ya watu kwa bomu la nyuklia, ukiwapo uwezekano mkubwa sana wa maangamizi ya viumbe vyote vyenye uhai juu ya sayari hii.

Amani ile inayopatikana kutokana na hofu yetu ya kuangamizana sisi kwa sisi imeonekana kwamba ni pungufu kuliko ile iliyo kamilifu tunayoitafuta. Hata pamoja na tishio la kuangamizwa wote kwa mabomu hayo ya nyuklia, dunia yetu imeshuhudia mapambano mengi madogo ya silaha, na vita kubwa kadhaa, kama zile za Korea, Vietnam, na Afghanistan. Mataifa hayo makubwa, yote mawili, - Urusi na Marekani - yakiwa yamevunjika moyo, yamejiondoa katika vita hizo ambazo hayakuweza kushinda kwa kutumia silaha za kawaida peke yake, lakini ambazo katika hizo waliingiwa na hofu ya kuweza kuliachilia lile jini kubwa la nyuklia kufanya kazi yake.

Katika jitihada hiyo inayovunja moyo ya kutaka kuleta umoja wa aina fulani pamoja na matumaini kwa ulimwengu huu alipiga hatua ndefu na kuingia mtu mmoja maarufu na mwenye mamlaka akitoa suluhisho kwa mahitaji ya wanadamu waliyo nayo kwa ajili ya amani na utulivu wa jamii. Katika mwezi wa Oktoba wa mwaka 1978, askofu wa Polandi asiyejulikana sana, Karol Wojtuyla, alichaguliwa kuwa kiongozi wa dini ya Kanisa la Katoliki na Mtawala wa Mji wa Vatikani. Papa huyu wa sasa ni dhahiri anaitumia nafasi yake ya uongozi kwa pande zote mbili [dini na serikali] katika juhudi yake ya kutekeleza imani yake kwamba yeye ndiye papa atakayerejea katika kiti cha enzi cha utawala wa ulimwengu huu, kiti cha enzi ambacho mapapa

walilazimishwa kukiacha katika mwaka ule wa 1798 mwisho wa Zama zile za Giza. Wengi wanamfikiria kwamba yeye ni papa wa kwanza wa kizazi hiki cha sasa aliye na uwezo wa kulitekeleza lengo kama hilo.

Kichwa kidogo cha kitabu kilichochapishwa hivi karibuni cha *The Keys of This Blood* [Funguo za Damu Hii] (toleo la jalada jepesi) kilitangaza mfululizo wa matukio yaliyokusudiwa ili kuifanyia mageuzi dunia hii ambayo yatadumu milele. Kiliwasonda kidole wahusika wakuu katika matukio hayo na lengo lao la mwisho. Kichwa kidogo cha kitabu hicho kinasomeka hivi: "Papa Yohane Paulo II dhidi ya Urusi na Nchi ya Magharibi [Marekani] wakiwania kutawala katika huo Mpango Ulimwengu Mpya."

Mwandishi, Malachi Martin, Mjesuti, azijuaye siri za ndani ya Vatikani, anachukua mtazamo wake unaopendelea pambano la upapa katika vita hii ya kuutawala ulimwengu mzima. Kitabu hicho kinatoa unabii fulani kuhusu siku za usoni za ulimwengu huu, na kufafanua sana juu ya mkakati wa Vatikani wa kuitawala dunia hii.

Mmojawapo wa unabii huo unaeleza kwa kinaganaga mkakati alionao papa wa kuufutilia mbali Muungano wa Kisovieti wa Urusi (U.S.S.R.) Kutimizwa kwa unabii huo hivi sasa ni historia iliyoandikwa vizuri. Magazeti ya ulimwengu yameonyesha kwa usahihi sehemu aliyotenda papa huyo katika kuusambaratisha Ukomunisti kama ishara yake ilivyoonekana katika kuangushwa chini kwa ule Ukuta wa Berlin tarehe 9 Novemba, 1989.

Sasa kwa vile Muungano wa Kisovieti wa zamani umekuwa ni sehemu tu ya historia, wahusika wakuu waliobaki

katika vita hii ya kuongoza na hata kudhibiti hali ya baadaye ya wanadamu wote ni Marekani (U.S.A.), Umoja wa Mataifa na Papa Yohane Paulo II. Lakini mpaka sasa bado haijaonekana iwapo China ya Kikomunisti itakuwa na mpango au itadhihirisha ajenda yake ya kuitawala dunia hii kisiasa.

Kwa sababu mwandishi mmoja tu wa Kijesuti anatabiri kwamba Mpango wa Ulimwengu Mpya umekaribia sana kutekelezwa, hilo halitoshi kutufanya sisi kuwa na wasiwasi usiostahili. Jambo moja linaloleta wasiwasi sana kuhusu mambo hayo yaliyotolewa kujadiliwa katika kitabu hicho cha *The Keys of This Blood* ni kwamba yanalandana kwa karibu mno na unabii ule ulioandikwa katika Biblia kwa zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Je, ni kwa umbali gani papa, Marekani na/au Umoja wa Mataifa watajisikia kuwa wanalazimika kuleta utulivu kwa hayo mapambano [ya silaha] yaliyomo humu duniani leo ambayo yanaonekana kuwa hayana mwisho? Ni njia zipi zitakazochukuliwa katika jitihada ya kuleta amani katikati ya hali ya sasa isiyotulia, kijamii, kisiasa, na kidini, ambayo imo ulimwenguni humu? Je, huo Mpango wa Ulimwengu Mpya au Serikali, utaanzishwa katika siku zetu hizi katika jitihada ya kuirejesha hali ya utulivu linganifu iliyokuwamo katika dola zile kuu za ulimwengu zilizopita? Sisi hatujaachwa katika hali ya kukisia-kisia tu kuhusu hoja hizi muhimu. Historia na Unabii vinaungana pamoja kutupatia mambo fulani ya kushangaza sana na maono mazito ya matukio hayo yatakayoitikisa dunia hii ambayo hivi sasa yako **mbele yetu na mbele ya ulimwengu mzima**.

Family Development International

P. O. Box 17

Mafinga/Iringa, Tanzania